Nipashe
Jumamosi Juni 13, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580257
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

## Wafanyakazi saba TPA mahakamani wakishtakiwa kusababisha hasara bil. 8/-

UKURASA 3






UKURASA 11



Katibu Mkuu wa CCM, Bashiru Ally.

# Kivumbi Urais CCM

## YATANGAZA ratiba ya mchakato kupata wagombea Bara na Zanzibar, Juni 15....*Endelea ukurasa 2*

### BAA LA CORONA



Wafanyakazi wanaouza maduka ya vyakula kupimwa joto siyo tija. Homa ni kati ya dalili za Covid-19 na kutokuwa na homa sio kigezo cha kutokuwa na maambukizo. Lazima kuwapo na miongozo kazini na mfanyakazi anapojisikia kupata dalili aripoti mara moja kwa uongozi. WHO

* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## WALIA KUKOSEKANA MZUNGUKO FEDHA

UKURASA 4

## BAJETI MBADALA:

# Waliopoteza ajira wapewe fao upotevu

UKURASA 3




**MICHEZO** YANGA, MWADUI HATUMWI MTOTO UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Kivumbi Urais CCM uchaguzi mkuu

**Na Mary Geofrey**

CHAMA CHA Mapinduzi (CCM), kimetangaza ratiba ya mchakato wa kupata wagombea urais wa Tanzania Bara na Zanzibar, itakayoanza Juni 15, mwaka huu.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, alitangaza ratiba hiyo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema mchakato wa urais wa Tanzania Bara utaanza na uchukuaji fomu, kuanzia Juni 15 hadi 30, mwaka huu utakaoendana na utafutaji wa wadhamini mikoani.

"Ndani ya siku 15 mgombea wa CCM atakuwa na kazi ya kuchukua fomu na kutafuta wadhamini mikoani na akamilishe kwa muda huo," alifafanua Polepole.

Pia, alisema baada ya mchakato huo, kitakachofuata ni vikao vya uchujaji majina ya wagombea, vitakavyoanza Julai 6 hadi 7, mwaka huu.

Alisema kikao cha Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, kitaanza mchakato wa uchujaji wa majina ya wagombea urais kuanzia Julai 8, mwaka huu na kuwasilisha kwenye kikao cha Kamati ya Usalama na Maadili ya chama hicho.

Kadhalika, alisema Julai 9, mwaka huu, Kikao cha NEC kitafanyika na kutoa mapendekezo ya majina matano ya wanachama wote walioomba kugombea nafasi hiyo kwa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM.

Polepole alisema Julai 10, mwaka huu, NEC itapendekeza majina matatu ya wanachama walioomba kugombea nasafi hiyo kwa mkutano mkuu wa CCM.

Kwa mujibu wa Polepole, kuazia Julai 11 hadi 12, mwaka huu, mkutano mkuu wa CCM Taifa, utachagua jina moja la mgombea wa urais wa Tanzania.

**MCHAKATO ZANZIBAR**

Kuhusu ratiba ya mgombea urais wa Zanzibar, Polepole alisema itaanza Julai 15 hadi 30 ya kuchukua fomu na kutafuta wadhamini mikoani.

Alisema ratiba hiyo itaanza Julai mosi hadi 2, mwaka huu kwa vikao vya sekretarieti ya Kamati Maalumu ya Halmashauri Kuu ya Taifa Zanzibar.

Pia, Julai 3 kitakaa kikao cha Kamati ya Usalama na Maadili Zanzibar na kuongeza kuwa ratiba itakayofuata ni kikao cha Kamati Maalumu ya Halmashauri Kuu ya CCM kitakachokaa Julai 4, mwaka huu, kwa ajili ya kutoa mapendekezo ya wanachama waliojitokeza kuomba kugombea urais wa Zanzibar.

"Kikao hicho kitafuatiwa na kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri ya Taifa kitakachokaa Julai 9, mwaka huu, kwa ajili ya kupendekeza majina matatu ya wanachama wanaoomba kugombea kiti hicho," alibainisha Polepole.

Kuanzia Julai 10, mwaka huu, alisema Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM itachagua jina moja la mgombea na Julai 11 hadi 12, Mkutano Mkuu wa CCM Taifa, utakaa kwa ajili ya kuthibitisha jina la mwanachama atakayesimama katika uchaguzi wa urais Zanzibar, kupitia chama hicho.

**WAGOMBEA WAONYWA**

Chama hicho kimetoa tahadhari kwa washiriki wa ugombea wa nafasi hizo kuwa wanyenyekevu na kutojihusisha na vitendo vya rushwa wakati wakisubiri kuteuliwa na chama.

Alisema wamefanya kikao na Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Brigedia John Mbungo, kwa ajili ya kuweka mikakati ya kushirikiana na chama kuwakamata wagombea watakaojihusisha na rushwa.

Alitahadharisha wagombea watakaojihusisha na vitendo vya rushwa watakatwa majina yao na hawatapata nafasi ya kuwania kupitia CCM wala vyama vingine vya siasa.

"Naendelea kusisitiza kuwa wagombea wa CCM waendelee kuwa na nidhamu ya hali ya juu wakati wote, wajishushe na siyo kujipeleka mbele wakati wote, ili chama chenyewe ndio kiseme kuwa huyu ni hodari na bingwa anaweza kusimama kuwania nafasi hiyo," alisema Polepole na kuwataka wagombea kujitathmini.



Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakari Zuberi, akizungumza na waumini wa dini ya kiislam baada ya swala ya ijumaa katika msikiti mkuu wa Gadafi, jijini Dodoma jana, ambapo aliipongeza serikali kwa kuwasilisha bajeti ya mwaka 2020/2021, anayolenga kuwajali Watanzania wenye kipato cha chini, pia amezifungua madrasa zote zenye wanafunzi wanaojitambua na kuwataka kuchukua tahadhari zote dhidi ya maambukizo ya ugonjwa wa corona. Kushoto kwake ni Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu. **PICHA: PETER MKWAVILA**.

# Upinzani waja na bajeti mbadala ya trilioni 23/-

***Waanika vipaumbele vitano wakitaka ajira na nyongeza ya mishahara...***

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni, imewasilisha bajeti mbadala ya Sh. trilioni 23.646 kwa mwaka wa fedha 2020/21, ikiweka vipaumbele katika sekta tano za elimu, kilimo, afya, viwanda na maji.

Akiwasilisha bungeni jana maoni ya kambi hiyo kuhusu hali ya uchumi wa taifa, Mpango wa Taifa wa Maendeleo na makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, Halima Mdee, alisema bajeti mbadala imejikita katika uhalisia wa uchumi wa ndani.

Mdee ambaye pia ni Mbunge wa Kawe (Chadema), alisema bajeti hiyo pia imejikita katika uchumi wa dunia na kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imefanya rejea ya makusanyo halisi ya mapato ya ndani na kufanya tathmini ya utekelezaji halisi wa bajeti za serikali kwa miaka minne iliyopita na kufikia uamuzi wa kupanga bajeti mbadala kwa kuzingatia uhalisia huo.

Alisema kambi hiyo pia imezingatia madhara ya janga la corona ambalo limetikisa uchumi wa dunia na hivyo kufikia uamuzi kushusha makisio yake ya bajeti kwa kuwa janga hilo limefanya mwelekeo wa uchumi kuwa na mserereko wa kushuka badala ya kupanda.

"Mbali na mlipuko wa corona, kulitokea pia mafuriko makubwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu katika kipindi cha mvua za masika, jambo ambalo limesababisha maafa na athari kubwa katika sekta mbalimbali za uchumi hususani sekta za kilimo na uchukuzi kutokana na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara na reli.

"Kwa kuwa wastani wa makusanyo halisi ya mapato kwa miaka minne iliyopita ni Sh. trilioni 26.273, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepunguza kiasi hicho kwa asilimia 10 na kufikia kiwango cha bajeti ya Sh. trilioni 23.646, ili kuzingatia madhara ya Covid-19.

"Kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarejea ushauri wake kuwa serikali kufanya marekebisho ya bajeti yake, ili iendane na uhalisia huo. Vinginevyo utekelezaji wa bajeti utakuwa mgumu kwa kuwa msingi wake hauna uhalisia kama ilivyoelezwa katika hotuba hii," alisema.

Katika mchanganuo wa bajeti mbadala Mdee alisema mapato ya kodi yatakuwa Sh. trilioni 15.125; mapato yasiyo ya kodi Sh. trilioni 1.775; mapato ya halmashauri Sh. bilioni 517.798 (hivyo jumla ya mapato yote ya ndani ni Sh. trilioni 17.418); misaada ya kibajeti kutoka nje Sh. bilioni 935.622; na mikopo ya ndani na nje Sh. trilioni 5.293.

Alisema matumizi ya kawaida ni Sh. trilioni 16,463 yakijumuisha Deni la Taifa Sh. trilioni 7.004, mishahara ambayo ni asilimia 25 ya bajeti mbadala Sh. trilioni 5.911, matumizi mengineyo asilimia 15 ya bajeti mbadala Sh. trilioni 3.547 na matumizi ya maendeleo (fedha za ndani na nje) Sh. trilioni 7.183.

Alisema vipaumbele ni elimu Sh. trilioni 4.729 (asilimia 20), kilimo Sh.trilioni 3.547 (asilimia 15), afya Sh. trilioni 3. 547 (asilimia 15), viwanda Sh. trilioni 4.729 (asilimia 20), maji Sh. trilioni 2.365 (asilimia 10) na sekta nyinginezo Sh. trilioni 4.729 (asilimia 20).

Mdee pia alisema kambi hiyo inaitaka serikali ilipe madeni ya mifuko ya hifadhi ya jamii, ili wastaafu walipwe mafao yao na pia kuiwezesha mifuko kujiendesha.

Alisema kuwa, kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya 2018/19 kuhusu utendaji wa mifuko, ni kwamba Mfuko mpya wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) haujafanya tathmini ya hali ya mali na madeni (actuarial valuation); na pia kumekuwapo madai ya muda mrefu ya Sh. bilioni 171.91 ya michango katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na PSSSF.

HABARI KITAIFA

## JANGA LA CORONA

# Waitaka serikali kuwalipa walimu 90,000 shule binafsi

## *Bunge nalo laingilia kati likitaka...*

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni, imeitaka serikali kulipa Fao la Kukosa Ajira kwa wafanyakazi wote ambao wamekidhi vigezo vya kisheria, wakiwamo waliopoteza ajira kutokana na janga la corona.

Akiwasilisha bungeni jana maoni ya kambi hiyo kuhusu hali ya uchumi wa taifa, Mpango wa Taifa wa Maendeleo na makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, James Mdee, alisema tangu kuingia kwa corona nchini, taasisi binafsi, zikiwamo shule binafsi zilisimamisha ajira.

Alisema kuwa kwa mujibu wa taarifa kutoka Chama cha Walimu wa Shule Binafsi, janga la corona limesababisha walimu 89,475 kusimamishwa kazi na hivyo hawalipwi mishahara.

"Kwa hiyo, serikali itumie Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi kuwalipa watumishi wote waliokosa ajira na ambao wamekidhi vigezo vya kisheria fao la kukosa ajira, ili waweze kumudu maisha yao," alisema.

Suala la walimu kusimamishwa kazi pia liligusiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ambayo katika taarifa yake ilisema Tanzania ina shule binafsi zaidi ya 2,750 zilizoajiri walimu takribani 90,000.

"Mtikisiko wa Covid-19 umedhihirisha umuhimu wa serikali kuchukua hatua mahsusi kunusuru shule hizo kwa kuahirisha malipo ya kodi na kuhimiza benki kutoa mikopo ya bei nafuu kwa shule hizo ili kuzijengea uwezo kulipa mishahara ya walimu wao.

"Aidha, Sheria ya Elimu inayozinyima shule hizo uwezekano wa kuweka akiba ya kutumia kulipa mishahara wakati wa dharura iangaliwe upya," alisema Mashimba Ndaki, Mwenyekiti wa Kamati hiyo alipowasilisha taarifa ya kamati yake bungeni jana.

**SAKATA LA KIKOKOTOO**

Katika hatua nyingine, Mdee alisema kambi yao serikali ni kuongeza mishahara ya wafanyakazi ambayo haijaongezwa kwa muda wote wa miaka mitano ya serikali ya awamu ya tano.

"Licha ya kutotekeleza wajibu huo wa kisheria, imekwenda mbali zaidi na kuingilia mafao ya wafanyakazi kwa lengo la kuyapunguza, ili wafanyakazi waishi maisha ya dhiki baada ya kustaafu utumishi wao serikalini.

"Hakuna asiyefahamu sakata la marekebisho ya kikokotoo cha mafao ya wastaafu baada ya mifuko ya hifadhi ya jamii kuunganishwa.

"Kimsingi sheria ile ya kikokotoo bado hijafanyiwa marekebisho. Alichokifanya Mheshimiwa Rais, ni kuahirisha matumizi ya sheria hiyo kwa kuisogeza mbele hadi mwaka 2023 ndipo kikokotoo kipya kianze kufanya kazi.

"Kambi Rasmi ya Upinzani inatafsiri kitendo hicho kama hadaa na danganya toto kwa wafanyakazi, ili waichague serikali ya CCM kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, lakini baada ya hapo tatizo liko palepale.

"Athari za kutofanya marekebisho ya kikokotoo cha mafao ya wastaafu katika sheria zimekuwa kubwa katika utumishi wa umma.

"Kwa mujibu wa taarifa ya CAG, watumishi wengi wanaomba kustaafu mapema kabla ya umri wa kisheria wa miaka 60, ili wanufaike na kikokotoo cha zamani cha mafao yao, ambacho kinatumika sasa kwenye kipindi cha mpito kabla kikokotoo kipya kinacholalamikiwa hakijaanza kutumika mwaka 2023," Mdee alisema.



Wafanyabiashara ndogo wakifanya shughuli zao chini ya Transfoma la umeme mkubwa katika eneo la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambalo ni hatari kwa maisha yao. **PICHA: JUMANNE JUMA**



## Mufti atangaza kufunguliwa rasmi madrasa

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MUFTI wa Tanzania Sheikh Abubakar Zuberi, ametangaza kufunguliwa rasmi kuanzia jana kwa madrasa, zilizofungwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (Covid 19).

Sheikh Zuberi, alitoa kauli hiyo jana jijini Dodoma wakati alipokuwa akizungumza na waumini wa dini ya Kiislamu katika msikiti wa Gadafi mara baada ya swala ya Ijumaa.

Alisema kuwa madrasa zote zilizofungwa zifunguliwe na kuanza kutoa huduma kama ilivyo kuwa awali, lakini kwa kuzingatia maelekezo ya wataalam wa afya.

"Lakini katika hili madrasa zitakazorudi na kuanza kutoa huduma ni zile pekee zenye wanafunzi ambao umri wao kidogo ni mkubwa na wanaojitambua, wale wadogo kabisa zitaendelea kufungwa mpaka hapo tena tutakapo toa tamko jingine," alisema Mufti Zuberi.

Kadhalika, alisema kuwa madrasa zitakazofunguliwa kuanza kazi zinatakiwa kuchukua tahadhari zote ambazo zinaelekezwa na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

"Lazima katika madrasa hizi kuzingatia maagizo ya wataalam kama vile kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa maji yanayotiririka na sabuni na hili sisi kama Waislamu hatutashindwa kwa kuwa Muislamu na kunawa ni jambo la kila siku," alisema.

Alipongeza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kufanikisha kupitisha bajeti kuu ya serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21.

# Wafanyakazi 7 TPA washtakiwa kusababisha hasara bil. 8/-

**Na Rose Jacob, MWANZA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imewafikisha mahakamani waliokuwa wafanyakazi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) wakikabiliwa na makosa sita ikiwamo ya kuisababishia serikali hasara ya Shilingi bilioni nane.

Pia, inawasaka mwanasheria wa kujitegemea wa kampuni ya Mnengele & Associated na kampuni ya ELA Advocates an Mnengere & Associates ya jijini Dar es Salaam, Arnold Temba na mfanyabiashara, Chrispin Irangue.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Kaimu wa Takukuru Mkoa wa Mwanza, Daudi Ndyamukama, watuhumiwa saba ambao ni watumishi wa TPA wameshafukuzwa kazi.

Alitaja makosa yanayowakabili kuwa ni kula njama kutenda kosa, kughushi, kuunda genge la uhalifu, kuwasilisha nyaraka za uongo, kuisababishia TPA hasara na utakatishaji wa fedha haramu.

"Takukuru kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka tutawafikisha mahakamani watuhumiwa hao wanane ambao walikuwa wanachunguzwa na makao makuu," alibainisha Ndyamukama.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Deogratius aliyekuwa Mhasibu mwandamizi TPA makao makuu, Bellian Lema, aliyekuwa Mhasibu mwandamizi TPA makao makuu, Aike Mapuli, aliyekuwa Ofisa uhasibu TPA makao makuu, Marystella Minja, aliyekuwa Mhasibu wa kituo cha Bandari Mwanza, Thomas Akile.

Wengine ni aliyekuwa Mhasibu msaidizi wa kituo cha Bandari Mwanza, Ibrahimu Lusato, aliyekuwa Mhasibu wa kituo cha Bandari ya Mwanza, Wendelin Tibuhwa, aliyekuwa Ofisa kodi wa kituo cha Bandari ya Mwanza, James Mbedule na wakili wa kujitegemea katika kampuni tajwa, Leocard Pendo.

"Pamoja na hatua hizi uchunguzi wa Takukuru bado utaendelea kwa lengo la kubaini kiasi kingine cha fedha kilichohujumiwa ikiwa ni pamoja na kuwatafuta na kuchukua hatua za kisheria kwa watuhumiwa wengine waliohusika na tuhuma hizi," alifafanua.

Vile vile, Takukuru imewataka wananchi kutoa taarifa zitakazosaidia kupatikana kwa watuhumiwa ambao hawajapatikana na kuahidi zawadi nono kwa atakayefanikisha kupatikana kwao.

# Waeleza kilio bajeti kukosekana mzunguko wa fedha

**Na Waandishi Wetu**

WASOMI, wanaharakati na wananchi wametoa maoni kuhusu bajeti iliyowasilishwa juzi bungeni na kueleza kilio cha kukosekana kwa fedha kwenye mzunguko.

Walisema matumaini yao makubwa ilikuwa ni kuona fedha nyingi ikielekezwa kwenye miradi itakayowezesha fedha kuwapo kwenye mzunguko, lakini imeelekezwa kwenye miradi mikubwa ya kimkakati.

Mhadhiri wa Uchumi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Profesa Honest Ngowi, alisema pamoja na bajeti hiyo kuonyesha ahueni katika mambo mengi, lakini bado nguvu kubwa imeelekezwa kwenye miradi mikubwa ya kimkakati.

Alisema bajeti kuweka nguvu kubwa katika miradi mikubwa ni jambo jema, lakini ni vyema ingepunguzwa nguvu kidogo na kuongezwa katika huduma za jamii ambazo wananchi wananufaika moja kwa moja.

"Kuweka nguvu katika miradi mikubwa ni jambo jema, lakini wananchi wanachotaka ni kuona namna gani watafaidika na miradi hiyo," alisema na kuongeza:

"Wananchi wa kawaida wanasema pesa imepotea mtaani, walitegemea kusikia kwamba sasa pesa inarudi kwa namna gani, wanataka kunufaika moja kwa moja."

Kuhusu viwanda vya ndani kupewa kipaumbele zaidi, Profesa Ngowi alisema ni jambo jema, lakini kuna haja ya serikali kuchukua tahadhari zaidi ili kuhakikisha kwamba vinafanya kazi kwa jitihada na ubora ili bidhaa zitakazozalishwa zilete ushindani katika soko la nje.

"Unajua kuna faida na hasara katika kulinda viwanda vya ndani, wakati mwingine tunaweza kulinda viwanda vyetu vya ndani halafu vikafa au vikashindwa kufanya kazi kama vile tulivyolenga au kukusudia na hivyo kuleta athari kubwa kwa wananchi na uchumi wa nchi, kwa hiyo kunahitajika umakini na tahadhari kubwa sana,"alisema Profesa Ngowi.

Alisema: "Lakini pia kama vitafanya vizuri itakuwa ni faida kwa nchi, kuna haja ya kuhakikisha vinaleta ushindani au kuzalisha bidhaa ambazo zitafaa na kuleta ushindani katika soko la nje pia."

Kwa mujibu wa mchumi huyo, kwa bajeti hiyo kuweka msisitizo wa kulinda viwanda vya ndani kutatengeneza ajira kwa kiwango kikubwa.

"Nipongeze kuendelea kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji kwa kuzingatia 'blue print' hususani kwa kuondoa kodi nyingi. Kupunguza ushuru kwa mlaji, kutasaidia kuleta ajira na kuchangia kwenye kodi, hili ni jambo zuri na ni neema katika kuweka mazingira mazuri ya biashara,"alifafanua Profesa Ngowi.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, aliipongeza serikali kwa kulinda viwanda vya ndani, huku akitaka usawa wa kijinsia kupewa kipaumbele kwenye viwanda kwa kunufaisha makundi yote.

Kadhalika, alisema bajeti hiyo imebebwa kwa kiasi kikubwa na vyanzo vya ndani badala ya kutegemea vya nje, huku kukiwa na kipaumbele kwenye afya, elimu na kuomba nguvu ya kupeleka maji vijijini iendelee kuongezwa kwa sababu bado kuna uhitaji.

**TAULO ZA KIKE**

Liundi alisema ni vyema kama bajeti hiyo ilivyoondoa kodi kwenye taulo za watoto ikatoa au kuondoa kodi kwenye taulo za kike ili kuwawezesha wengi kuzinunua kwa bei rahisi na kuwawezesha kuingia darasani bila kikwazo.

"Tunaendelea kutilia mkazo kwamba taulo za kike ziondolewe kodi, pamoja na msisitizo ambao umewekwa kwenye viwanda, vitengwe ambavyo vitafanya kazi ya kutengeneza taulo hizo ili angalau ziuzwe chini ya Sh. 1,000 kupunguza mzigo kwa mtoto wa kike," alisema Liundi.

**BAJEI ELIMU**

Naye, Ofisa Mipango wa Idara ya Utafiti na Uchambuzi wa Sera wa HakiElimu, Judith Kapinga, alisema changamoto zilizopo katika sekta ya elimu hazilingani na kiwango cha bajeti kilichotengwa.

Alisema bado kuna uhaba wa walimu, ukosefu wa vyumba vya madarasa vya kutosha, mabweni na matundu ya vyoo ambavyo kwa ujumla wake vinahitaji fedha nyingi kuliko bajeti iliyopo.

Kapinga alisema kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, bajeti katika sekta ya elimu imekuwa ikipungua badala ya kuongezeka.

Naye, Mkurugenzi wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema bajeti hiyo kwa asilimia kubwa ni nzuri imefuta kodi na tozo mbalimbali, lakini bado haijafikia matamanio ya Watanzania.

Alisema bajeti hiyo pia imeonyesha kuwapo kwa mwamko mkubwa wa ulipaji kodi ingawa serikali imeshindwa kufikia lengo la kukusanya Sh. trilioni 33.1, lakini ikakusanya asilimia 93.

Kwa mujibu wa Olengurumwa, bajeti hiyo ni ya kujiendesha yenyewe bila kutegemea misaada kutoka mataifa mengine na kwamba juhudi za ukusanyaji kodi zikiendelea watafikia lengo la makusanyo kwa mwaka ujao ambayo ni Sh. trilioni 34.88.

Kadhalika, alisema mambo ambayo hawajayasikia ni kuhusu mikakati ya kurejesha hali ya uchumi ulioyumba kutokana na kuwapo kwa janga na Covid -19.

"Sawa wameelezea athari za kuwapo kwa corona lakini hawajaeleza mikakati ya kurejesha hali ya uchumi kwa sababu biashara zimefungwa, shule na shughuli nyingine za kuwaingizia Watanzania vipato," alisema Olengurumwa.

Naye, Johnson Alli, mkazi wa Ilala, jijini Dar es Salaam, alisema: "Naipongeza serikali kwa kuboresha sekta ya ardhi kwa kuhifadhi taarifa za upimaji na umiliki wa ardhi kwa njia ya kielektroniki kwa kuwa itasaidia kupunguza migogoro ya ardhi kwa Watanzania."

***Imeandikwa na Elizabeth Zaya, Mary Geofrey na Mauld Mbaga (DAR), Grace Mwakalinga (Mbeya)**



Mafundi wakikarabati kipande cha barabara kwenye makutano ya mtaa wa Sikukuu na Twiga, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**.

## Matatani shtaka kusafirisha dawa za kulevya

**Na Hellen Mwango**

MKAZI wa Dar es Salaam, Ashrafu Hamisi, amefikishwa mahakamani akikabiliwa na shtaka la kusafirisha kilo 21.7 za dawa za kulevya.

Mshtakiwa huyo alisomewa shtaka lake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Janeth Magoho, ulidai kuwa, Julai 13, 2019 katika eneo la Kinondoni, mshtakiwa akiwa na wenzake Ramadhan Gumbo, Fahadi Salehe na Hassan Gumbo, walikutwa akisafirisha dawa za kulevya aina ya heroin.

Washtakiwa wenzake walisomewa mashtaka yao Julai 25, 2019.

Hakimu Shaidi alisema kesi hiyo itatajwa Juni 17, mwaka huu na mshtakiwa amepelekwa mahabusu.

# JPM ateta na Waziri Mkuu wa India

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, jana alifanya mazungumzo na Waziri Mkuu India, Narendra Modi, katika masuala yahusuyo uhusiano na ushirikiano wa kirafiki na kihistoria uliopo kati ya nchi hizo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu Chamwino, katika mazungumzo hayo ambayo Waziri Mkuu huyo alimpigia Rais Magufuli, kiongozi huyo wa India alimtakia heri kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Alimhakikishia kuendeleza kukuza uhusiano na Tanzania katika nyanja mbalimbali hasa kiuchumi, huku akimpa mrejesho wa yaliyojiri katika mkutano wa nchi 20 tajiri duniani (G20), uliofanyika hivi karibuni.

Alimweleza kuwa nchi hizo zimekubaliana kuwa taasisi za fedha za kimataifa zitoe msamaha wa madeni kwa nchi masikini na zinazoendelea, zilizopata madhara ya corona.

Rais Magufuli ameipongeza India kwa juhudi za kutafuta chanjo ya corona ambazo anaamini zitafanikiwa na kwamba Tanzania ikiwa moja ya nchi zilizokumbwa na ugonjwa huo itanufaika, japo ugonjwa wenyewe unapungua kwa kasi kubwa hapa nchini.

Pia, alimshukuru kwa uhusiano na ushirikiano mzuri wa Tanzania na India ambayo ni miongoni mwa nchi tano zinazoongoza kwa uwekezaji hapa nchini.

Alishukuru kwa mikopo nafuu inayotolewa na India kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa nchini.

Aliitaja baadhi mikopo kuwa ni wa ujenzi wa Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, mikopo ya miradi ya maji na ufadhili wa masomo ya elimu ya juu kwa wanafunzi wa Tanzania wanaokwenda kusomea masuala ya afya, uhandisi na Tehama nchini India.

"Mikopo ya miradi ya maji ni pamoja na Sh. bilioni 225.9 (Ruvu- Dar es Salaam, ambao umekamilika), Sh. bilioni 611.5 (Maji ya Ziwa Victoria kwenda Tabora, Nzega na Igunga ambao unakaribia kukamilika)."

"Sh. trilioni 1.2 (miradi ya maji ya miji 28, ambayo utekelezaji wake unaendelea) na Sh. bilioni 209.9 (miundombinu ya maji ya Zanzibar, ambayo inaendelea kujengwa)."

# Siku ya Kimataifa wenye ualbino

## • PWA yalia kunyanyapaliwa

Na Elizabeth Zaya

WATU wenye ualbino (PWA), wamesema bado kundi hilo linakabiliwa na changamoto kubwa ya kunyanyapaliwa katika jamii na kuomba kuendelea kupambana kukomesha vitendo hivyo.

Kwa mujibu wa taaifa iliyotolewa na PWA kwenye vyombo vya habari jana, vitendo hivyo vinasababishwa kwa kiwango kikubwa na imani potofu ambayo bado jamii inayo dhidi ya kundi hilo.

Taarifa hiyo ilitolewa na kundi hilo, ikiwa ni maadhimisho ya Kimataifa ya Uelewa kuhusu Ualbino (IAAD) ambayo hufanyika Juni 13, kila mwaka.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kutokana na tishio la janga la ugonjwa wa corona, maadhimisho hayo yanafanyika kupitia vyombo vya habari huku Shirika la Under The Same Sun (UTSS), likiitumia siku hiyo kutoa elimu inayolihusu kundi hilo kupitia vyombo hivyo vya habari.

"Ni ukweli usiopingika na inajulikana hadharani kwamba watu wenye ualbino, wanakabiliwa na aina nyingi za ubaguzi ulimwenguni kwa sababu hali hiyo bado haijapokelewa na kueleweka katika kijamii," ilifafanua taarifa hiyo.

"Mara nyingi imani potofu na zinazoongozwa na imani za ushirikina, ndizo zinazochochea kutengwa kwao katika jamii, hii inasababisha aina tofauti za unyanyapaa, ubaguzi, na hata mauaji."

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, ndilo lilipitisha azimio linalotaka kuzuia na kukomesha mashambulio na ubaguzi dhidi ya kundi la watu wenye ualbino.

Walitoa wito kwa mashirika mengine ya asasi za kiraia kuendelea kutetea haki za kundi hilo pamoja na mengine yenye mahitaji maalum.

Ilieleza kuwa pamoja na mabadiliko na maboresho kadhaa yanayofanyika nchini yanayohusu kundi hilo, bado hakuhitajiki kupuuza changamoto hizo zinazoendelea kuwakumba.

Kaulimbiu ya maadhimisho inasisitiza haki sawa kwa wote, kuboresha afya, elimu na ajira kwa watu wenye ualbino.

Pia walisisitiza kuboresha huduma za jamii na ustawi wa kundi hilo.




Meneja wa NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi (wa pili kushoto), akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, msaada wa vifaa vya kunawa mikono vyenye thamani zaidi ya Sh. milioni moja ili kujikinga na maambukizo ya corona, nje ya ofisi ya mkuu huyo Manispaa ya Singida juzi. Kushoto ni Meneja wa NMB tawi la Singida, Willy Mponzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Singida ataka usimamizi misaada

Na Mwandishi Wetu

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, amewataka wakurungenzi wa halmashauri kusimamia mali na misaada inayotolewa na wadau mbalimbali wa maendeleo nchini, ili itumike vizuri na kwa malengo iliyokusudiwa.

Akizungumza kwa nyakati tofauti wakati akipokea misaada kutoka Benki ya NMB mkoani hapa, Dk. Nchimbi alisema misaada hiyo ni sehemu ya maendeleo yao wananchi na walengwa wengine hivyo ni jukumu la viongozi wa maeneo husika kuzisimamia ili kutumika kwa vizazi vijavyo.

NMB jana walikabidhi madawati 100 kwa ajili ya shule mbili za Wilaya ya Mkalama pamoja na vifaa vya kunawa mikono.

"Tumekuwa na kawaida ya kupokea misaada ya vifaa vingi katika maeneo yetu, lakini hakuna ufuatiliaji wake, nawataka wakurungenzi wote wa halmasahauri kuhakikisha mnazisimamia mali hizi ili zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa," alisema Dk. Nchimbi.

Vilevile, aliomba taasisi zingine kuinga mfano wa benki ya NMB nchini kwa kutenga sehemu ya fedha zake na kusaidia kupunguza changamoto katika jamii.

Akikabidhi misaada ya madawati, Meneja Uhusiano na serikali wa Benki ya NMB, Josephine Kulwa, alisema benki hiyo imekabidhi msaada wa madawati 100 yenye thamani ya Sh. milioni 10 ikiwa ni kurudisha faida katika jamii kwa kuwaunga mkono benki hiyo.

Alisema, msaada huo ni juhudi za benki hiyo kuunga mkono serikali kuwahudumia wananchi kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Kulwa alibainisha kuwa madawati hayo ni kwa ajili ya shule za msingi Yulansoni na Miganga, kila moja itapata madawati 50.

Awali, wakati wa kukabidhi vifaa vya kunawa mikono kutoka NMB ofisini kwa Mkuu wa mkoa, Dk. Nchimbi, Meneja wa NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema jamii iendelee kujenga tabia ya kunawa mikono kila wakati ili kujikinga na corona na magonjwa mengine ya kuambukiza.

# Wabunge 26 wahojiwa tuhuma ubadhirifu

Na Renatha Msungu, DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imewahoji wabunge 26 kati ya 69 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kuhusu tuhuma za ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka ndani ya chama hicho.

Miongoni mwa wabunge waliohojiwa ni pamoja na Peter Lijualikali, Suzan Lyimo, Frank Mwakajoka, Lucy Mollel, Joseph Haule, Suzan Kiwanga, Paschal Haonga, Godbles Lema na Hawa Subira.

Wengine ni Risala Kabongo, Gimbi Masaba, Julius Kalanga, Antony Komu, Mary Muro, Rhoda Kunchela, Japhary Michael, David Silinde, Joseph Mbilinyi, Mchungaji Peter Msigwa, Esther Bulaya, Halima Mdee na Esther Matiko.

Nipashe ilishuhudia mahojiano hayo kuanzia juzi kwa wabunge 11 kuhojiwa na jana walihojiwa wabunge 15.

Akizungumza baada ya kutoka katika mahojiano hayo, Mbunge Lijualikali alisema mahojiano yalikuwa mazuri, lakini hakuna jipya kwa kuwa aliyoulizwa ni yale aliyozungumza bungeni kuhusu ubadhirifu huo na viongozi wa Chadema.

Aliwataka wabunge wenzake kuongea ukweli watakapokwenda katika mahojiano hayo kwasababu Takukuru imejipanga na wanajua kila kitu, wanachotaka ni uthibitisho kutoka kwao.

Kwa upande wake, Mbunge Silinde alisema taasisi hiyo imejipanga hivyo hakuna sababu ya wabunge kusema uongo kwa sababu wataumbuka. Alisema hakuna vitisho wakati wa mahojiano hivyo wasiwe na wasiwasi, waende wakaseme ukweli.

Hivi karibuni Ofisa Uhusiano wa taasisi hiyo, Doreen Kapwani, alisema mahojiano hayo yanafanywa kwa wanachama na wale waliowahi kuwa wanachama kuhusu ubadhirifu huo.

Alisema hatua hiyo ni mwendelezo wa uchunguzi wa taasisi hiyo kuhusu malalamiko yaliyotangazwa na wabunge waliokihama chama hicho ambapo walidai kukatwa mishahara yao kila mwezi kuanzia Juni 2016.

Kwa mujibu wa malalamiko hayo, wabunge wa viti maalum walikuwa wakikatwa kiasi cha Sh.1,560,000 na wabunge wa kuchaguliwa kwenye majimbo walikuwa wanakatwa Sh.520,000 na hawafahamu matumizi yake.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Lala salama Ligi Kuu Tanzania Bara ivutie*

**BAADA** ya Rais Dk. John Pombe Mafuguli kutangaza kuifungulia rasmi michezo hapa kuanzia Juni Mosi, mwaka huu, Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea tena nchini kuanzia leo.

Ligi Kuu ndiyo itakayoanza kuchezwa, kati ya ligi nyingine zinazofanyika nchini, kwa sababu ya kutaka kukamilisha msimu wa mwaka 2019/20 na hatimaye kupata mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano yajayo ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), timu zitakazoshuka dimbani kuanza kusaka pointi tatu muhimu ni zile ambazo zilikuwa na mechi za viporo.

Mechi hizo ni kati ya Mwadui FC ya Shinyanga itakaowakaribisha Yanga kutoka jijini Dar es Salaam na Namungo FC itakuwa ugenini Tanga kuwavaa wenyeni Coastal Union, mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara mwaka 1988.

Mpaka Ligi Kuu inasimama, Simba yenye pointi 71, ndio walikuwa vinara katika msimamo, wakati Singida United inaburuza mkia ikiwa na pointi 15.

Ligi hiyo pamoja na Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili, Ligi Kuu ya Wanawake na Ligi Kuu Zanzibar, zilisimama kwa zaidi ya miezi miwili ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19).

Kutokana na janga hilo, wachezaji wa ligi hizo wote walikuwa wakifanya mazoezi binafsi ili kulinda viwango vyao kwa kufuata programu maalumu walizopewa na makocha wao na sasa kuanzia kesho, watashuka dimbani kuendelea na kampeni ya kuwania ubingwa unaoshikiliwa na Simba.

Haya hivyo, wanamichezo na wadau wote watakaoshiriki michezo hiyo, watatakiwa kuendelea kufuata maelekezo ya kujikinga na corona kama ambavyo wataalamu wa afya wanavyoelekeza ili kuendelea kubakia salama wakati na baada ya kumaliza mchezo.

Angalizo hili limetolewa na serikali kwa sababu ya kuendelea kuwalinda wananchi wake na janga hilo lililotikisa duniani.

Nipashe inawatakiwa wachezaji wote kuendeleza nidhamu kufuata na kuheshimu kanuni, sheria na taratibu zilizowekwa katika kila mechi hasa katika kipindi hiki cha lala salama.

Timu itakayokuwa na nidhamu, itajiweka katika nafasi nzuri ya kutimiza malengo yake huku ikiwakumbusha kutokata tamaa kwa wale walioko kwenye janga ya kushuka daraja kwa sababu bado mechi hazijamalizika.

Katika michezo na hasa soka, si vema mchezaji au timu ikakata tamaa wakati mechi hazijachezwa na wanachotakiwa kukifanya ni kupambana hadi pale filimbi ya mwisho itakapopulizwa.

Hata wale walioko katika mbio za ubingwa, nao watatakiwa kufahamu hakuna ambaye ameshakamilisha msimu, timu mojawapo kati ya tano zilizoko kwenye nafasi ya juu kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha klabu 20, inaweza kutangazwa mabingwa.

Nipashe pia tunazikumbusha timu nane zilizobakia kwenye mashindano ya Kombe la FA, kuendelea kujiimarisha na kati ya hizo, yoyote inaweza kutwaa ubingwa na hatimaye kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.


Katika dunia ya sasa, hakuna timu ndogo, mechi zote zilizobakia za kuanzia hatua ya robo fainali, zina uzito sawa na ili kupata matokeo chanya, kila timu inatakiwa kumheshimu mpinzani wake.

Tunawakumbusha wachezaji na viongozi, wakati huu wa lala salama ni muhimu kwa sababu pia hutoa taswira ya kuelekea msimu mpya na ndio kipindi cha wachezaji kujituma na kujihakikishia thamani ya juu kwenye dirisha la usajili ambalo tayari limeshaanza kufunguka ingawa sio rasmi.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge

# *Michezo ni burudani*



Na Barnabas Maro

**'BURUDANI'** ni hali ya mtu kufarijika kutokana na kupata au kuona kitu anachokipenda. Ni mambo yanayofanywa ili kuchangamsha watu; starehe.

'Mchezo' ni jambo ambalo watu au timu hulifanya kwa kushindana ili kupata ushindi. Pia ni kazi ya sanaa ambayo huigizwa kwa ajili ya kuelimisha na kuburudisha watu. Jambo ambalo mtu au watu hulifanya kwa kupitisha wakati au kujifurahisha; masihara.

'Ushindani' ni tabia ya kupambana kwa maneno au vitendo bila kupigana. 'Ushinde' ni tendo la mtu kukiri kushindwa kama vile mitihani au michezo. 'Ushindi' ni hali ya mtu kufanikiwa katika jambo alilokuwa akiliwania.

'Ushindwaji' ni hali ya mtu kutofanikiwa katika jambo alilokuwa akilipigania.

Ndo maana wahenga walisema "Asiyekiri ushinde hakuwa mshindani." Maana yake mtu asiyekubali baada ya kushindwa si mshindani. Methali hii hutumiwa kuwanasihi binadamu kukubali wakishindwa au kuukiri udhaifu wao. Kwa hiyo asiyekubali kushindwa si mshindani.

Kati ya michezo inayovuta halaiki (idadi kubwa ya mkusanyiko wa watu; umati. Sanaa ya maonyesho inayochezwa na watu wengi) ni mchezo wa mpira wa miguu, au unaweza kuita soka, kandanda au kabumbu.

Mchezo huo huzikutanisha timu mbalimbali kushindania kitu fulani kama ngao, kikombe au hata hela. Kabla timu hazijakutana uwanjani, kila moja hufanya mazoezi yatakayoisaidia kuwashinda wapinzani wao na kutwaa zawadi inayoshindaniwa.

Pamoja na mazoezi, pia wachezaji hupewa mbinu mbalimbali za kucheza ili kupata ushindi. Moja ya mbinu hizo ni nidhamu, yaani mpangilio maalumu wa kufanya jambo; adabu ya mtu mbele ya wengine.

Mchezaji anayecheza rafu, yaani jambo linalofanywa kinyume na kanuni zinazotawala mchezo, huadhibiwa kwa mujibu wa sheria za mchezo. Huonywa kwa kuoneshwa kadi ya njano.

Walimu wa mpira wanapaswa kuwasisitizia wachezaji wao umuhimu wa kuwa na nidhamu kuanzia majumbani mwao, mitaani na viwanjani wanapokuwa kwenye mashindano.

Vilevile wawashauri wachezaji kujiepusha na ulevi, sigara, ukware, na uraibu (kitu ambacho mtu kajenga mazoea ya kukitumia) wa mihadarati (dawa za kulevya).

Mchezo wa kandanda una faida mbili muhimu kwa wachezaji: kwanza unajenga miili yao kwa kuwa na afya bora kutokana na mazoezi ya viungo. Pili hulipwa mishahara mizuri na tatu huwaburudisha watazamaji wanaotoa fedha zao ili kuburudishwa na mchezo usio na vurugu.

Mfano mzuri ni wachezaji wa timu mbalimbali za Ulaya na Marekani wanaolipwa mishahara mikubwa kuliko wanazolipwa viongozi wa nchi wanazotoka.

Huko wapo wachezaji walionunua ndege au meli, wachilia mbali msururu wa magari ya kifahari ya aina mbalimbali, saa na simu za bei kubwa, bila kutaja majumba kadhaa ya kifahari.

Twaweza kuchukua mfano mdogo tu kwa Mbwana Samatta, Mtanzania anayecheza kandanda la kulipwa Uingereza hivi sasa.

Sisemi kuwa wachezaji wetu walio Ulaya na Marekani waige upuuzi wa kuwa na msururu (safu ya vitu vilivyokaa kimoja baada ya kingine) wa magari kama wenzao, hasha.

Watanzania watakaopata bahati ya kusajiliwa na timu za ughaibuni, waanzishe miradi yao humu nchini itakayowanufaisha si wao tu, bali Watanzania na nchi kwa jumla badala ya kujitafutia ufahari*. Wawe na hekima, yaani maarifa ya kufanya jambo kwa ufanisi; busara.

Tukiacha hayo, leo Jumamosi Yanga itaanza na viporo vyake dhidi ya Mwadui ugenini na kukutana na JKT Tanzania Jumatano ijayo pia ugenini. Coastal Union (Wagosi wa Kaya) wataikaribisha Namungo kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Kesho Jumapili Simba ambao wana nafasi nzuri ya ubingwa Ligi Kuu kwa mara ya tatu mfululizo, itawakaribisha Ruvu Shooting jijini Dar es Salaam. Azam FC watakuwa wenyeji wa Mbao FC ya Mwanza kwenye uwanja wao wa nyumbani uliofanyiwa ukarabati mkubwa.

Jumatano ijayo, JKT Tanzania wakiwa uwanja wa nyumbani watawakaribisha Yanga ili kumaliza viporo vyao vilivyosababishwa na maambukizo ya ugonjwa wa covid-19, maarufu kwa jina la corona.

Juni 20, 2020 timu 12 zitapambana. JKT Tanzania watakuwa wenyeji wa Singida United, Ndanda wataikaribisha Biashara ya Mwanza na Namungo watakuwa nyumbani kupambana na wageni wao, Kagera Sugar.

Coastal Union (wagosi wa kaya) watakuwa nyumbani kupambana na wageni wao, Mtibwa Sugar. Polisi Tanzania watakuwa wenyeji wa Lipuli FC huku Mbeya City wakiwakaribisha Alliance.


***marobarnabas@yahoo.com***
***0784 334 096***

HABARI KITAIFA

# Watanzania waliokwama Saudia warejeshwa

Na Mary Geofrey

SERIKALI imewarejesha Watanzania 146 waliokwama nchini Saudi Arabia, kufuatia kusitishwa kwa safari za ndege za kimataifa kutokana na kuwapo kwa mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19.

Taarifa iliyotolewa juzi na Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Emmanuel Buhohela, ilieleza kuwa Watanzania hao walirejea nchini jana na Shirika la Ndege la Arabia.

Alisema ndege hiyo iliondoka kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jeddah saa 2:30 asubuhi na kuwasili katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere saa 7:20 mchana, juzi.

"Kupitia utaratibu huu, hadi sasa jumla ya Watanzania 671 wamefanikiwa kurejea nchini kati ya waliokuwa wamekwama katika nchi mbalimbali.

Kati yao 119 walirejea nchini kutokea Oman, 101 walitokea kwa ndege zilizochukua raia wa kigeni nchini na Watanzania watano walirejea kwa ndege ya mizigo ya Shirika la Ethiopian kutoka Misri," alisema Buhohela.

Alisema pia wizara inaratibu safari za raia wa kigeni kwenda katika nchi zao na hadi kufikia Mei 17, mwaka huu, jumla ya raia wa kigeni 1,172 na Watanzania 44 waliondoka kwenda nchi mbalimbali.

Buhohela alisema wizara kupitia Balozi za Tanzania kwenye nchi husika imeendelea kuratibu kazi ya kuwarejesha nyumbani Watanzania wengine 1,165 waliokwama kwenye nchi mbalimbali duniani.

"Wizara imeziagiza balozi zote za Tanzania nje ya nchi kuratibu kazi ya kukusanya taarifa na orodha ya Watanzania waliokwama katika maeneo ya uwakilishi ili kutumia fursa ya ndege zinazokuja kuchukua raia wa kigeni nchini," alieleza Buhohela.

# Madiwani waridhia mtendaji kufukuzwa kazi

Na Stevie chindiye, TUNDURU

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma, limeridhia kufukuzwa kazi Ofisa Mtendaji wa Kata ya Daraja la tatu, anayetuhumiwa kwa utoro kazini.

Makubaliano hayo yalifikiwa kufuatia mjadala uliofanyika katika kikao cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2019/2020, kilichoketi mjini hapa.

Akisoma taarifa hiyo baada ya baraza hilo kugeuzwa kama kamati na baadaye kufikia maazimio hayo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Mbwana Sudi, alisema uamuzi huo umefuatia tabia za jeuri zilizoonyeshwa na mtendaji huyo.

Sudi alifafanua kuwa kabla ya uamuzi huo mtumishi huyo alipewa notisi mbili, ya kwanza ilitolewa Oktoba 10, mwaka jana na nyingine Februari 5, mwaka huu za kumtaka ajieleze kwanini haendi katika kituo chake cha kazi, lakini hakuzijibu.

Alisema kitendo hicho ni ukiukaji wa sheria ya utumishi wa umma namba 45 (1) cha kanuni ya adhabu namba 42 (1) A hadi C vya utumishi wa umma na marekebisho yake ya mwaka 2009, vinavyo waelekeza madiwani kupendekeza mtumishi kushushwa cheo ama afukuzwe kazi.

Baada ya Mwenyekiti kusoma maelekezo hayo ya kisheria na baadaye kuwahoji, madaiwani kwa pamoja waliridhia kufukuzwa kazi kwa mtumishi huyo.




Malori mawili yakiwa yameanguka kando ya Barabara ya Mwai Kibaki, eneo la Mbezi Beach, jijini Dar es Salaam jana. Chanzo cha ajali hiyo hakikufahamika. **PICHA: SALOME KITOMARI.**

# Jukata yataka uchaguzi mkuu ushirikishe wenye ulemavu

Na Elizabeth Zaya

JUKWAA la Katiba Tanzania (Jukata), limewasilisha kwa Msajili wa vyama vya siasa, changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu katika utungwaji wa sera ya ushiriki wa kundi hilo kwenye siasa.

Jukata iliwasilisha changamoto hizo juzi ilipofanya mazungumzo na Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungu, jijini Dodoma.

Katika mazungumzo hayo, Jaji Mutungi alizitaka asasi za kiraia, kuandaa, kubadili mtazamo uliopo kwa jamii kuhusu watu wenye ulemavu hususani katika ushiriki wao kwenye siasa na mambo mengine.

"Kama tunataka kuongelea ushiriki wa watu wenye ulemavu, twendeni huko katika familia zao kuona matatizo yao," alisema Jaji Mutungi.

Alishauri ni vyema kuingiza ajenda za ushiriki wa kundi hilo katika masuala mbalimbali yakiwamo ya siasa na kuwachagua kutokana na uwezo wao.

Pia, aliitaka Jukata kupeleka ajenda za kizalendo kwa usahihi katika jamii na kwa makundi ya watu wenye ulemavu.

Mshauri Mwelekezi wa Jukata, Deus Kibamba, alisema lengo la kukutana na Msajili ni kuwasilisha changamoto mbalimbali zinazolikabili kundi la watu wenye ulemavu hususani katika masuala ya siasa.

"Tuliona nafasi ya Msajili ni muhimu hasa katika kukuza demokrasia na malezi ya vyama siasa, ndiyo maana tunaona tuzungumze naye ili tumpe mawazo juu ya ushiriki wa makundi maalum," alisema Kibamba.

"Tulifanya uchambuzi kuonyesha hizo changamoto katika siasa za Tanzania ambazo zinaonyesha kuna ushiriki duni wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu."

Kibamba aliiomba ofisi ya Msajili iratibu wizara inayohusika na sera, kwenye utungwaji wa sera ya ushiriki wa makundi hayo maalum.

Kibamba alisema vipo vikwazo kadhaa vinavyowakabili wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ikiwamo fedha za kampeni, siasa chafu na uteuzi duni wa makundi hayo ndani ya vyama.

Alishauri kuwe na ushirikiano kati ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Tume ya Taifa Uchaguzi Tanzania (NEC) na Ofisi ya Msajili ili kuongeza vigezo vya usawa wa kijinsia.

Mwenyekiti wa asasi ya Ushiriki Tanzania, Israel Ilunde, alisema ili kufanikisha kampeni ya siasa safi na ushiriki wa wananchi, ni muhimu kuwekeza zaidi katika elimu ya uraia kwa jamii.

# 'Acheni kuzika eneo la ranchi'

**Na Lilian Lugakingira,** MISSENYI

WAKAZI wa Wilaya ya Missenyi, mkoani Kagera wametakiwa kufuata sheria zilizowekwa na halmashauri zinazowakataza kuzika maeneo yaliyokatazwa kisheria yakiwamo ya Ranchi ya Taifa ya Missenyi na maeneo ya mipango miji ili kuepuka kuingia katika migogoro na serikali na kuhatarisha amani.

Akizungumza wakati wa kufunga rasmi Baraza la Madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo, Mkuu wa wilaya hiyo, Kanali Denis Mwila, alisema kuwa serikali inalazimika kufukua makaburi katika maeneo ya ranchi hiyo kutokana na baadhi ya wananchi wa Kata ya Kakunyu, kukaidi agizo la kutozika maeneo hayo.

"Kuna wakati mwingine tulikinzana na madiwani maana uamuzi mwingine aliyokuwa akiyachukua viongozi hawa wa kuchaguliwa waliona nawaharibia kura, lakini kila mtu na kazi yake, wao wameaminiwa kuwawakilisha wananchi, lakini kwa sababu ni lazima sheria itekelezwe ilibidi iwe hivyo ili isionekane hakuna serikali," alisema.

Alisema kwa muda wa wiki mbili zilizopita, walilazimika kwenda kufukia kaburi lililokuwa limechimbwa katika eneo la Kasambya kwa ajili ya kuzika, kutokana na baadhi ya wananchi kutotii sheria.

"Katika sheria zilizopitishwa na madiwani, Kasambya ni eneo la mipango miji kwa hiyo ni marufuku kuzika huko, taarifa zilitoka kwa wananchi kuwa kuna watu wanataka kuzika tukawakataza, lakini hawakusikia, tulienda tukafukia kaburi," alisema.

Alisema baada ya kufukia kaburi hilo wakaingia katika mgogoro na wananchi na kuleta mitazamo tofauti, lakini wanachopaswa kukifahamu wananchi hakuna mtu yeyote aliyeko juu ya sheria, awe mwenye pesa au mnyonge.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Wilaya ya Missenyi, Abdalah Mayomba, alisema halmashauri hiyo haiko vizuri katika mipango ya matumizi mazuri ya ardhi na kushauri Baraza la Madiwani lijalo kufanyia kazi suala hilo ili kuepusha migogoro pia kuboresha mapato yake kupitia idara hiyo.

"Kwenye suala la matumizi ya ardhi halmashauri yetu haiko vizuri, nina uhakika wengi wenu mtachaguliwa na mtarudi, basi mtakaporudi mwendeleze mipango mizuri ya matumizi ya ardhi," alisema.

Akisoma taarifa ya Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya hiyo anayemaliza muda wake, Projestus Tegamaisho, Diwani wa Kata ya Nsunga, Yasi Katunzi, alilitaka baraza lijalo kuainisha vyanzo vipya vya mapato ili kuwezesha mapato ya halmashauri kupanda na kuiwezesha kutekeleza miradi ya maendeleo ya wananchi kwa kutumia vyanzo vya ndani.

"Tunatarajia ifikapo mwaka wa fedha 2024/2025 halmashauri ikusanye zaidi ya Sh. bilioni tano kutokana na vyanzo vyake vya ndani vya mapato, kwa kuwa na kiasi hicho halmashauri itapunguza utegemezi kutoka serikali kuu kwa zaidi ya asilimia 40 katika shughuli za uendeshaji wa ofisi na miradi ya maendeleo," alisema.



Mafundi wakijenga msingi kwa ajili ya jengo la wodi ya mama na mtoto la zahanati ya kijiji cha Bukima, wilaya ya Musoma, mkoani Mara juzi, ikiwa ni moja ya mikakati ya kuboresha huduma za afya katika zanahati hiyo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Tanapa yaombwa kuondoa tembo wasumbufu

**Na Restuta Damian,** KYERWA

MAMLAKA ya Hifadhi ya Tanzania (Tanapa), imeombwa kuondoa tembo kwenye mashamba ya wananchi wa Kata Businde, wilayani Kyerwa, mkoani Kagera na kupelekwa wanapostahili.

Diwani wa Viti Maalumu wa kata hiyo, Consolata Kanyima, amesema tembo hao wanashambulia vijiji vya Businde na Bugela na kusababisha wananchi kuhama.

Alisema ni kipindi cha miaka mitano tangu Tanapa walipofika na kueleza watafanya uondoaji huo.

Vile vile, Kanyima alisema tembo huingia kwenye mashamba na kufanya ushambuliaji wa mazao.

"Wameshambulia maeneo hadi wananchi wamehama kwenda vitongoji vingine kuwapisha tembo, wameacha mashamba tunaomba watolewe watu warudi," alisema Kanyima.

Diwani wa Kata Songambele, Majaliwa John, alisema shughuli za wananchi zimekwama kutokana na eneo lililotegemewa kwa kilimo kuvamiwa.

John alisema, mwezi Machi wataalam wa Tanapa walitembelea eneo hilo na kuahidi kuondoa wanyama kwa kusaidia wananchi.

Kwa upande wake Kamshina wa hifadhi za Taifa pori la Ibanda, Kyerwa na Rumanyika, Murondo Murondo, alikiri kuwapo kwa changamoto hiyo.

Murondo alisema, hatua iliyochukuliwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti Wanyama Pori (TAWIRI) walitembelea eneo hilo na kubaini idadi ya tembo kati ya 80 hadi 100.

Alisema, njia ya kuwaondoa ni kuwagawa kwa makundi matatu ambayo yatapita kwenye mashamba ya wanachi.

"Kama tunafahamu tembo ni mnyama wa porini na huwa hasahau njia yake ni tofauti na wanyama wa kufugwa kwamba watafukuzwa taratibu," alisema Murondo.

"Labda kuwaambia tu wananchi wasiwabugudhi hadi watakapopelekwa eneo la hifadhi ndiko sehemu sahihi," alisema Murondo.

Alisema Hifadhi ya Ibanda Kyerwa kuna vijiji 19 na Rumayika vipo 16 ambavyo vimezungukwa na hifadhi ya pori hilo.

Alisema mara nyingi wanyama pori huingia sehemu ambayo sio eneo lao na kufuata eneo ambalo limetulia.

# Serikali kuwezesha makundi Maalum 10% ya mikopo

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

SERIKALI imeahidi kuendelea kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili waweze kujiajiri na kujiinua katika shughuli zao za kiuchumi kwenye jamii na kuongeza pato la serikali.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Ofisa Maendeleo wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Vicent Msola, wakati akizungumza na baadhi ya wenyeviti wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, ambao wanashirikiana na Shirika la Elimisha kuwaibua wasichana wasiokuwa na ajira ili waweze kupatiwa mafunzo ya kujiongezea kipato.

Alisema kama serikali inapongeza uamuzi wa shirika hilo kuja na mbinu ya kuwasaidia wasichana wasio na ajira kuwajengea maarifa ya kujiongezea kipato katika ngazi ya familia.

"Serikali inatambua umuhimu wa hatua ya Shirika hilo la Elimisha kuja na mkakati wa kutoa elimu na mafunzo ambayo yatachangia wasichana hao kujiajiri na kuendesha shughuli endelevu za kiuchumi, pamoja na kuondokana na hali ya umaskini katika ngazi ya familia," alisema Msola.

Alisema uamuzi wa shirika hilo kutoa elimu ya kujikwamua na umaskini utasaidia kundi kubwa la wasichana majumbani ambao hawana ajira ya kujikwamua na hali ya umaskini inayowakabili kutokana na wengi wao kutokuwa na utamaduni wa kujishughulisha kiuchumi.

Alisema mafunzo hayo yatawasaidia kukidhi mahitaji yao ya msingi yakiwamo mahitaji ya chakula kutokana na fedha watakazozipata kutokana na kufanya kazi.

Msola alisema, baada ya wasichana hao kupatiwa mafunzo ya kujiongezea kipato, serikali imejipanga kuangalia uwezekano wa kuwasaidia wasichana hao kwa kuwakopesha fedha zinazotolewa na halmashauri kwa ajili ya makundi ya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

"Baada ya wasichana hao kupatiwa mafunzo na kuwa na shughuli ya kujipatia kipato, serikali itawasaidia kwa kuwapatia mkopo wa fedha wa asilimia 10 zinazotolewa na halmashauri," alisema Msola.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Ilemi, Mwanaisha Rashid, alisema watahakikisha wanashirikiana na shirika hilo kuwatambua wasichana katika mtaa wao ambao wanauhitaji wa kupewa mafunzo ya kujiongezea kipato.

# Wataka vijana kulindwa dhidi mimba za utotoni

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

CHAMA Cha Wabunge wa Masuala ya Watu na Maendeleo nchini (TPAPD), kimeiomba serikali kuweka mifumo ya kusimamia maadili ya vijana ambao wapo nyumbani kwasasa ili wasiwe waathirika wa ngono zembe na kuongezeka kwa mimba za utotoni.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti wa chama hicho, Jamal Kassim, ambaye pia ni Mbunge wa Magomeni (CCM), katika semina ya wabunge hao iliyolenga kuhamasisha, kuweka kipaumbele, na kuwekeza kwenye uzazi wa mpango wakati wa janga la ugonjwa wa corona.

Alisema mifumo hiyo inapaswa kuwapo kwasasa hasa ikizingatiwa vijana hao wapo nyumbani kutokana na janga hilo.

"Lengo kusiwe na wahanga wa ngono zembe, hata unyanyasaji wa kijinsia na kusababisha kuongezeka kwa mimba katika umri mdogo na utoaji mimba usio salama," alisema.

Hata hivyo, alitoa wito kwa wabunge waliopo madarakani na wale wanaowania kuingia bungeni baada ya uchaguzi mkuu kutoa kipaumbele katika suala la huduma, taarifa na vifaa vya huduma za uzazi wa mpango.

"Wahakikishe vinapatikana kiurahisi kwa wanawake na wasichana pindi kunapotokea majanga kama ilivyo wakati huu," alisema.

Kadhalika, alisema TPAPD inatoa wito maalum kwa wenye nia ya kugombea ubunge kuhakikisha masuala hayo yanapewa kipaumbele katika agenda za kampeni zao.

"Kwa wabunge wasio na nia ya kugombea nafasi za ubunge katika Bunge lijalo, TPAPD inatoa wito kwao kuendelea kuunga mkono uzazi wa mpango na afya ya uzazi ya mama, mtoto, rikabalehe, na vijana popote watakapokuwa,"alisema.

Aliwataka watakaobahatika kuingia bungeni kuchochea utekelezaji wa mipango hiyo huduma za uzazi wa mpango na afya ya uzazi wakati wote na katika ngazi zote.

Alisema chama hicho kinashauri kuwekwa kwa vipaumbele kwenye rasilimali na afua ili zihusishe taarifa za afya, huduma na vifaa vya huduma za afya ya uzazi ambazo zinazingatia rika na jinsia wakati wa majanga kama corona.

Alisema mpango wa pili wa taifa uliokasimiwa wa uzazi wa mpango 2019-2023,unasisitiza kuwekeza kwenye maeneo muhimu ikiwamo utoaji wa huduma za afya ya uzazi, uwezeshaji wa kijinsia na usawa kwenye upatikanaji wa huduma za afya.

Alisema kutokana na janga hilo, chama kinaamini serikali itandelea kuhamasisha upatikanaji wa bidhaa za huduma za afya ya uzazi na uzazi wa mpango kwa urahisi na haraka.



Diwani wa Kata ya Chamwino, Jumanne Ngede (kushoto), akizungumza na viongozi wa ngazi ya kata, mitaa na watendaji katika kikao cha kujadili utekelezaji wa ilani ya uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya 2015, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# 'Msishawishike rushwa, chagueni viongozi wazuri'

**Na Peter Mkwavila, CHAMWINO**

WANANCHI wa Wilaya ya Chamwino, wametakiwa kujiepusha na vishawishi vya rushwa ili kuwachagua viongozi bora.

Wito huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi(CCM), wilayani humo, Francis Gombo, alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa kupokea utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM mwaka 2015 uliyofanyika kata ya Buigiri.

Aliwataka watakapoona viashiria vyovyote vya rushwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), ili hatua zingine zichukuliwe.

Pia, aliwasishi kutochagua viongozi watakaotaka kupeperusha bendera kwenye magari yao, bali watakaokuwa tayari kuwapa maendeleo.

Aliwataka viongozi waliopo ngazi ya kata, vijiji na vitongoji kusimamia ilani hiyo kwa kuhakikisha miradi yote inakuwa chini ya uangalizi wao.

Nao, viongozi hao kutoka Chinangali, Mwegamile na Buigiri wilayani humo, wamewataka watakaojitokeza kuwania nafasi ya ubunge na udiwani kuhakikisha wanatekeleza ilani ya uchaguzi.

Awali, akisoma taarifa ya ilani hiyo, Diwani wa Kata ya Buigiri, Keneth Yindi, alisema katika kipindi cha miaka mitano, sekta ya elimu, afya, maji, nishati ya umeme na miundominu ya barabara imekuwa katika eneo hilo.

Yindi alisema pamoja na mafanikio hayo pia migogoro ya ardhi iliyokuwapo kati ya wananchi na Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, imetatuliwa na kuwarejeshea ekari 113 wakulima wa vijiji vya Mwegamile, Chinangali na Buigiri.

## Serikali yakamata kilo 66 dawa za kulevya

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imekamata kilogramu 65.69 za dawa za kulevya aina ya heroin na cocaine kwa mwaka 2019.

Pia, watuhumiwa 10,384 wamefunguliwa kesi mahakamani zikiwa kwenye hatua mbalimbali.

Hayo yalibainishwa juzi na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, alipokuwa akitoa taarifa ya hali ya dawa za kulevya kwa kipindi hicho.

Alisema Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, imepata mafanikio makubwa katika mapambano dhidi ya dawa hizo nchini kwa mwaka huo.

"Kwa kushirikiana na wadau wa nje na ndani ya nchi, imefanya operesheni mbalimbali ndani ya nchi ikiwamo mipakani na katika ukanda wa pwani na Bahari ya Hindi na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza uingizwaji wa dawa za kulevya nchini,"alisema.

Alisema katika kipindi hicho, kilogramu 55.35 za heroin, kilogramu 10.34 za cocaine, bangi tani 21.16 na tani za mirungi 9.07 zilikamatwa.

Alisema dawa zinazokamatwa huteketezwa kwa mujibu wa sheria kwa kushirikisha mamlaka mbalimbali za serikali baada ya hukumu kutolewa.

"Mwaka 2019 tuliteketeza kilogramu 122.55 za heroin na kilogramu 71.507 za cocaine katika viwanda vya saruji Dar es Salaam na Mbeya,"alisema.

Alisema kwa mwaka 2019, bangi ilitumika zaidi nchini na pia kumejitokeza ongezeko la matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya ikiwamo tramadol, ketamine, valium na nyingine kama mbadala wa heroin na cocaine.

Kadhalika, alisema ongezeko hilo lilichangiwa na udhibiti mkubwa wa dawa za kulevya zilizozoeleka kama heroin na cocaine unaofanywa na serikali.

"Waraibu wa dawa za kulevya wanapokosa dawa walizozizoea hukimbilia kutumia dawa tiba zenye asili ya kulevya ili kupunguza makali ya arosto wanayoipata," alisema.

Kwa upande wake, Kamishna wa Kinga na Tiba wa mamlaka hiyo, Dk. Peter Mfisi, alisema ipo sheria inayompa mamlaka Kamishna kuruhusu kilimo cha bangi au koki kwa ajili ya matumizi ya kisayansi kama tafiti au matumizi ya kutengenezea dawa.

# Baraza lashauri mfuko ZSSF kuwekeza miradi yenye tija

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameutaka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), kuwekeza katika miradi yenye tija ili kuepuka hasara na kufanya mfuko huo kupoteza mwelekeo na tishio la kufilisika.

Mwakilishi wa jimbo la Chake Chake, Suleiman Sarhani alisema mfuko wa hifadhi ya jamii ni miongoni mwa mikakati na malengo yake ni kujikita katika uwekezaji wa sekta mbalimbali ikiwamo miradi ya kiuchumi na majengo ya ofisi.

Alisema wasiwasi wake mkubwa ni baadhi ya miradi inayotekelezwa na mfuko huo kutoleta tija na matokeo mazuri kwa maendeleo ya mfuko ikiwamo ujenzi wa kiwanja cha kufurahisha watoto Tibirinzi, Pemba.

"Mheshimiwa Spika, nauomba uongozi wa mfuko wa hifadhi ya jamii kujikita katika uwekezaji wa miradi yenye tija ili kuepuka kuingia hasara na kutishia kufilisika," alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma, alipongeza uwekezaji wa mfuko huo ambao umejikita katika miradi ya ujenzi wa majengo ya kibiashara.

"Nimefurahishwa na uwekezaji wa miradi ya majengo ya biashara katika maeneo ya mji wa Unguja ambayo yanaweza kuleta faida kwa maendeleo ya mfuko na kuongeza mapato," alisema.

Naye Mwakilishi wa jimbo la Paje, Jaku Hashim Ayoub, aliutaka uongozi wa mfuko huo kujenga nyumba zenye gharama nafuu ambazo zitanunuliwa na wafanyakazi.

Alisema nyumba zilizojengwa na mfuko huo Mbweni Unguja ni za gharama kubwa na hakuna mfanyakazi wa kawaida mwenye uwezo wa kununua au kukodi kwa ajili ya kuishi.

"Mheshimiwa wakati umefika sasa mfuko wa hifadhi ya jamii ujenge nyumba nafuu zitakazonunuliwa na wafanyakazi ambao ndiyo wachangiaji wakubwa wa mfuko huo ili nao waweze kunufaika," alisema.

Kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, mfuko unaendelea kutekeleza miradi mitatu mikubwa ikiwamo ujenzi wa jengo la biashara eneo la Kisonge, lenye gharama za Sh. bilioni 12.4,pamoja na jengo lingine la biashara jirani na Thabit Kombo lenye gharama ya Sh. bilioni 4.6.

Alisema, mfuko huo unaendelea na ujenzi wa hoteli kubwa Mkoani Pemba kwa gharama za Sh. bilioni 3.6 ambayo itaruhusu watu mbalimbali wakiwamo wafanyabiashara kupata malazi ya uhakika.



Mwakilishi wa Jimbo la Dimani, Dk. Mwinyihaji Makame (kushoto), akijadiliana jambo na Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, nje wa ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani, Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Zaeca yatakiwa kuchunguza migogoro ardhi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAMLAKA ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (Zaeca), imetakiwa kuelekeza nguvu zake kuchunguza migogoro ya ardhi ambayo baadhi yake inawahusisha watendaji wa serikali na kusababisha malalamiko miongoni mwa jamii.

Mwakilishi wa Viti Maalumu Mkoa wa Kaskazini Unguja, Hidaya Ali Makame, alisema migogoro ya ardhi ikiwamo wakubwa kuchukua ardhi kwa ajili ya shughuli za uwekezaji, imewafanya wananchi wa kijiji hicho kuwa maskini.

"Tunaiomba Mamlaka ya kupambana na rushwa na uhujumu wa uchumi, kujikita kupambana na rushwa kwa kuwatafuta watu wanaojishughulisha na migogoro ya ardhi ambayo imezidi katika kijiji cha Nungwi," alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele, Ali Suleiman, aliitaka Mamlaka ya kupambana na rushwa kuacha kujishughulisha na kuwasakama wanasiasa peke katika kipindi hichi kuelekea uchaguzi mkuu, wakati kuna viongozi wanachukua maeneo ya ardhi za wananchi kwa nguvu kwa kutumia madaraka yao.

"Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi zaidi katika maeneo ya ukanda wa fukwe za baharini imeshamiri kwa kiwango kikubwa ikiwamo Kijiji cha Nungwi...tunaiomba Zaeca kujielekeza huko," alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae, Mohamed Said Dimwa, alisema wananchi wengi wa maeneo ya ukanda wa fukwe za baharini ni maskini kwa sababu hawakufaidika na ardhi kama rasilimali ya kuwaondoa katika unyonge.

"Tunawataka wenzetu wa Zaeca kuelekeza nguvu zao kuwatafuta watu wanaojiingiza katika migogoro ya ardhi na kuwadhulumu wanyonge," alisema.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroub Ali Suleiman, alisema

## Uandikishaji wapigakura wapya, uhakiki

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KAZI ya uandikishaji wapigakura wapya na uhakiki wa taarifa za waliomo katika Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa wilaya ya Mjini, imemalizika jana huku hali ya amani na usalama ikiwa imetawala katika vituo hivyo.

Akizungumza wakati akitembelea vituo vya uandikishaji, Ofisa Uandikishaji wa Wilaya ya Mjini wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), Safia Iddi Muhammad, alisema, mafanikio ya kazi hiyo yanatokana na mfuno mzuri ulioandaliwa na Tume hiyo ambao unawapatia huduma wananchi bila usumbufu.

Alisema kazi hiyo inaendelea kuendeshwa kwa misingi mizuri ya kitaalamu zaidi na kila taarifa za mpigakura huhifadhiwa na kuwekwa kumbukumbu katika mfumo wa Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Alisema, Tume baada ya kukamilisha taratibu za uandikishaji, inatarajia kuwapatia vitambulisho wananchi walioandikishwa ambavyo vitawawezesha kupiga kura katika uchaguzi mkuu.

Kwa upande wao Masheha katika vituo vya uandikishahaji, waliipongeza Tume hiyo kwa kuweka mfumo wa uandikishaji ambao unafanyakazi kwa haraka zaidi kwa kutumia wastani wa dakika moja mpaka mbili kumuandikisha mwananchi na kuhakiki taarifa za mpigakura.

Baadhi ya wakuu wa vituo vya uandikishaji walieleza jinsi walivyojipanga kuwapatia huduma wananchi wanaofika vituoni kupata huduma na kubainisha jinsi wanavyoyatumia mafunzo waliyopewa na Tume hiyo na kuzingatia maelekezo na mikakati iliyowekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kujikinga na maradhi ya Covid-19.

**Kwa upande wao Masheha katika vituo vya uandikishaji, waliipongeza Tume hiyo kwa kuweka mfumo wa uandikishaji ambao unafanyakazi kwa haraka zaidi kwa kutumia wastani wa dakika moja mpaka mbili kumuandikisha mwananchi na kuhakiki taarifa za mpigakura.**



MADEE ANOGEWA YANGA BUTU
Uk. 13



PINELA

# Wasanii wa kiume Bongo Fleva watatoka mate kwa sana

MWANAMUZIKI wa Injili ambaye ameibua utata kutokana na umbo lake la nyigu, Pinela, amesema anapata wakati mgumu kutokana na wanamuziki wa kiume wa Bongo Fleva, kummezea mate

Akizungumza hivi karibuni, Pinela, amesema kila wakati anakumbana na vurugu katika akaunti yake ya Instagram, baada ya wasanii hao kumpatia mialiko, huku wengine wakimuahidi kumpatia donge nono la fedha.

Hata hivyo, amesema kutokana na yeye kuwa mtumishi wa kweli wa Mungu, anawaambia ukweli kwamba haiwezekani kuwa nao karibu kwa jambo lolote, kwa kuwa lipo kinyume na imani yake.

Hata hivyo, amesema baadhi ya wanamuziki hao wamemtaka hata kuwa mpambaji wa video zao, lakini amewatolea nje.

Pinela, amesema yeye amechagua kumtumikia bwana kwa kutumia muziki, jambo la kuingia katika muziki wa Bongo Fleva litampa tabu na kuwachukiza wazazi wake ambao ni watu wa dini.

"Wasanii wa kiume wa BongoFleva wameshawahi kunifuata, tena walikuwa wanakuja na dau kubwa sana kuanzia Milioni 3 huko, ila mimi tayari nimeshaokoka, itakuwa ngumu kwenda huko, kwa hiyo siwezi kufanya kazi za kidunia" amesema Pinela.

Akizungumzia endapo akifuatwa na wasanii kama Harmonize au Alikiba, wakitaka kumtumia kwenye kazi zao mrembo huyo amesema

"Hapo pagumu na wote nawapenda ila sitaenda hata kwa mmoja, siwezi kufanya nao kazi kwa sababu mimi ni mtu wa injili wao wanafanya kazi za kidunia".

BASI SAWA

## Harmorapa hataki kuwa kondoo bhana!

MSANII aliyeibuka na kushuka kwa kasi kama mshumaa, Harmorapa, ameapa kutompigia magoti Harmonize, baada ya mwanamuziki huyo kumfungia katika akaunti yake ya Instagram.

Akizungumza na EATV, Harmorapa, amesema hatua hiyo ya kufungiwa na Harmonize lina historia ndefu na kwamba hawezi kulizungumzia kwa sasa.

"Siwezi kukaa kumuomba msamaha kwa sababu hakuna jambo nimemkosea, kwanza kila mtu ananyota yake na siwezi kutembelea nyota ya mtu, Mungu aliyeniumba mimi ndiye kamuumba yeye na watu wote, kwahiyo haiwezi kutokea kumuomba msamaha kisa nimetembelea nyota yake " amesema Harmorapa.



## Chidy hukujua kuwa ghali ni gharama?

MBUNIFU na Mfanyabiashara wa mavazi, Chidy Designs, ametumia siku sita pekee kuishi na mchumba wake, Jacqueline Wolper, kisha kuamua kubwaga manyanga.

Chidy amesema baada ya kuishi kwa siku hizo chache amegundua kuna vitu kati yao haviko sawa, licha ya kumsifia kuwa ni mwanamke anayejua kutafuta pesa.

"Labda niweke wazi mimi na Jack tulikuwa mtu na mchumba wake, katika wanawake ambao nimewahi kuwa nao amewazidi baadhi ya vitu kwa sababu anajua kuitafuta pesa kwa jasho lake mwenyewe na ameweka kazi mbele".

Akaongeza, "Kutokana na mazingira ambayo yupo nayo na mimi kazi zangu zinavyoenda, unakuta kuna vitu havipo sawa halafu mwisho wa siku kila mmoja kivyake, kuna kitu kimeingia na hakipo sawa baada ya pete ya uchumba tumeachana"





## Matonya, eti uvivu umekusaidia?

UVIVU ni jambo baya, katika jamii mtu akiwa mvivu anaonekana hafai, lakini kwa mwanamuziki Matonya, anasema tabia ya uvivu imempatia faida.

Matonya amesema, uvivu wake wa kutopenda kuonekana kwa watu, umemsaidia kwenye maisha yake na kumfanya kuwa kiwango cha juu kama alivyo sasa.

"Mimi nipo na napatikana, sio kama sitaki mazoea bali maisha ambayo ninayoyaishi ni ya kutulia sio kujificha, nikiwa sina vitu vya umuhimu naona bora nitulie nyumbani mara nyingi pia nakuwa na uvivu japo uvivu wangu unanisaidia, hata biashara zangu hazipaswi kuonekana kwenye macho muda wote" ameeleza Matonya.



## Madee anogewa Yanga butu

MSANII wa BongoFleva, Madee Seneda, ameibuka na kuwatetea wachezaji wa timu yake ya Yanga, akisema hawakuwa fiti kutokana na kukaa muda mrefu bila kucheza.

Yanga ambayo ilichezea kichapo kutoka kwa KMC, imekuwa na wafuasi sugu akiwamo Madee, ambaye anasema huwa hapati usingizi pale timu hiyo inapopoteza mchezo.

"Nahisi Yanga tumeangalia sana kwenye ligi, wachezaji walikuwa wamekaa kwa kipindi kirefu ndani hadi wengine tumeambiwa wameongezeka uzito na hawajaweza kuwa sawa, chochote kingeweza kutokea hata wakifungwa 9, hakuna lawama," amesema





## Imeanza Chameleone Uganda, imeishia kupagawisha Bongo

**Na Adam Fungamwango**

ANAITWA Dk. Jose Chemeleone, huku jina lake halisi likiwa ni Jaseph Mayanja. Ni mzaliwa na nchini Uganda. Huyu ni msanii maarufu sana si Afrika Mashariki na Kati tu, bali Afrika nzima kwa sasa.

Kitu kinachomtofautisha na wasanii wengine wa Uganda ni baadhi ya nyimbo zake kuimba kwa lugha ya kiswahili. Tena kiswahili fasaha.

Ndiyo maana Chalemeone ndiyo msanii ambaye anatambuliwa zaidi na kipenzi cha mashabiki wa muziki wa Tanzania.

Amejizolea mashabiki wengi nchini kutokana na si tu kuimba kiswahili, lakini hata ngoma zake anazotoa zimekuwa bora na kuwapagawisha watu.

Mara kwa mara amekuwa akitoa ngoma za kiswahili ambazo zimekuwa zikitamba sana kwenye redio na televisheni za Tanzania.

Hizi ni baadhi ya ngoma ambazo pamoja na kuwa ni Mganda, lakini zimemfanya uwe maarufu zaidi Tanzania.

**Shida za Dunia**

Hii ni moja ya ngoma za mwanzo kabisa zilizomtambulisha Dk. Chemeleone. Ilitoka mwanzoni mwa miaka ya 2000 na wengi walidhani kuwa ni msanii kutoka Tanzania kwa jinsi alivyoimba wimbo huu.

Ni wimbo unaozungumzia mtu mmoja akilia shida baada ya kupata matatizo ya kufukuzwa kazi na mkewe kumtoroka, lakini rafiki yake anamwambia aache kulia kwani ni shida tu za dunia na Mwenyezi Mungu anamjaribia, ipo siku mambo yatakaa sawa.

**Jamila**

Ni ngoma ambayo ilizidi kumuweka msanii huyo Mganda kwenye mioyo ya Watanzania.

Ngoma hii ilimzungumzia demu mmoja ambaye aliachwa na mpenzi wake na akawa ana majonzi makubwa na kububujikwa na machozi. Ili kupata ushauri nasaha alikwenda kwa Chameleone ambaye naye hakuwa na kazi nyingine ila kumbembeleza.

**Badilisha**

Katikati ya miaka ya 2000, Dk. Chameleone alikuja kivingine kwa kutoa ngoma yake kali aliyoiita 'Badilisha'.

Ngoma hii ilizidi kupata heshima nchini Tanzania, kiasi cha kuitwa mara kwa mara kwa ajili ya kutunukiwa tuzo kwenye mashindano ya muziki ya Kitanzania na ile ya kiswahili pia.

**Valuvalu**

Ni ngoma iliyopendwa na Wabongo wengi kuelekea mwishoni mwa miaka ya 2000. Ni wimbo wa mapenzi ambao Chameleone alikuwa akimwambia mpenzi wake kuwa anapenda awe wake na aachane wa watu valuvalu ambao hawapendi kuona mapenzi yao yanaendelea.

Ngoma hii ilizidi kumuweka msanii huyo mioyoni mwa Wabongo ambao hadi wapende ngoma yako uwe umefanya kazi kweli kweli.

**Tubonge**

Ngoma hii ndiyo ilifunga kazi kweli kweli. 'Tubonge' ni ngoma ambayo iko zaidi kwenye uelekeo ya wimbo wa 'gospel', yaani wimbo wa Injili. Lakini kwa jinsi ulivyopigwa ni kama bongo fleva tu, ila maneno yake ni ya Injili, hivyo baada ya kutoka ulikonga nyoyo za mashabiki wote wa muziki wa bongo fleva na Injili pia. Ukawa unapigwa kotekote, ukienda kwenye miziki ya kidunia upo na miziki wa kumuimbia Bwana unapigwa pia na watu wanaserebuka kama kawaida.

## Mwiko: Kupenda hupofusha macho

**Na Adam Fungamwango**

SIKUZOTE mapenzi ni ugonjwa. Anayependa haoni wala hasikii. Kwenye pengo huita kuna mwanya na kwenye chongo huona kuna kengeza.

Lakini pamoja na hayo yote, kupenda pia kuna mipaka yake. Huwezi kumpenda mke wa mtu, ndugu yako wa damu, au mtu mwenye nasaba naye. Na yoyote anayefanya hivyo, mwisho wake huwa ni majuto.

Filamu ya 'Mwiko' inathibitisha hili. Imechezwa na wasanii Mohamed Nurdin maarufu kama 'Chekibudi', Madebe Lidai, Anwar Nassao, Shasta na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha Maisara na Medebe ni mtu na mpenzi wake. Hata hivyo hilo linapingwa mno na familia ya kina Maisara ambao hawataki uhusiano huo, kiasi cha kumtisha Madebe. Mwisho wa siku anapigwa na kaka ya Maishara na kualazwa hospitalini.

Baada ya kutoka, kunakuwa na uhasama kati ya ukoo wa Madebe na Maishara. Ugomvi huo unasababisha hata lile wazo la Madebe kutaka kupeleka barua kwa mpenzi wake kufa.

Hiyo inampa fursa mzee mmoja kijijini hapo anayeitwa Jitikavu kupeleka ombi la kutaka kumuoa binti huyo. Pamoja na kwamba ana umri mkubwa na ana watoto ambao ni wakubwa kuliko binti huyo, lakini wazazi wa Maisara wanakubali haraka, kwanza wakitaka binti yao aolewe, lakini pia ni kama kumkomoa Madebe.

Ndoa inafungwa, lakini Madebe bado akili yake iko kwa Maisara. Kitendo hicho cha mara kwa mara kukutana na mpenzi wake wa zamani, kinamfanya mume mzee Jitikavu kutokuwa na amani. Mara kwa mara anakwenda nyumbani kwa Madebe kwenda kumuwekea mkwara.

Hatimaye Maisara anapata ujauzito. Anampa siri shoga yake kuwa ujauzito huo si wa mumewe mzee Jitikavu na wala si wa mpenzi wake Madebe. Wa nani?

Shoga mwenyewe naye mbea hatari. Maneno hayo anayapeleka kwa wahusika. Kiguu na njia hadi kwa Madebe na pia akamweleza yote mumewe mzee Jitikavu.

Akawa tayari ameshakaanga mbuyu, akawaachia wenye meno watafune. Mume na Madebe kila mmoja kivyake akawa anatafuta mimba hiyo ni ya nani?

Maisara akakutana na mpenzi wake aliyempa mimba ili wayapange. Shoga yake alikuwa ameshaijua sehemu hiyo, hivyo akawapa taarifa Jitikavu na Madebe.

Kila mmoja alifika na kumshuhudia Maisara akiwa na Anwar, mtoto wa mzee Jitikavu wa kumzaa mwenyewe. Kumbe ndiye mwenye mimba.

Kumbe pia binti huyo alikuwa na uhusiano wa kimapenzi wa Anwar tangu zamani, hivyo baba yake alipomuoa alikuwa kama amemsogezea hivi.

Medebe nguvu zilimuishia, akaamua kukaa chini. Mzee Jitikavu akaamua kumfukuza nyumbani mtoto wake na kumpa talaka mkewe Maisara.



# Juliet kuitwa 'chotara' hiyo dharau



MWIGIZAJI kutoka Ghana, Juliet Ibrahim, amekasirishwa kuitwa 'chotara',akiamini kuwa kutumia neno hilo ni sawa na kumdharau.

Juliet ambaye amezaliwa na mama raia wa Liberia na baba yake Mlebanon, amekuwa na rangi mchanganyiko jambo linalosababisha kuwa tofauti na waigizaji wengine wa kike.

Kumekuwa na mazungumzo kuhusu neno hilo linavyokasirisha Juliet kiasi cha kumfanya kuweka ujumbe mzito katika ukurasa wake wa Instagram, akilaumu kutambulishwa kwa kutumia jina hilo.



## Zoro nenda polisi kama kweli hujabaka

RAPA wa Nigeria, Owoh Chimaobi Chrismathner, maarufu kama 'Zoro', amekiri kuitwa na polisi baada ya kufunguliwa shitaka la ubakaji.

Katika barua ya wito kutoka kituo kikuu cha Polisi cha Logos, mwanamuziki huyo anadaiwa kosa hilo alilifanya mwaka 2015, ikielezwa alifanya mapenzi na msichana mdogo Yachit Ayuba, bila ridhaa yake.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, Zoro, amewaambia mashabiki wake kwamba yupo tayari kuchunguzwa kwa kosa hilo huku akiamini hana hatia kwani ametengenezewa kwa nia ya kumchafua.

## Duh! Tonto zawadi kama hiyo balaa

MREMBO kutoka kiwanda cha filamu cha Nollywood, Tonto Dikeh, amefurahia siku yake ya kuzawadiwa gari la kifahari.

Dikeh, ambaye ametimizia miaka 35, wiki hii amekabidhiwa gari aina ya Mercedes Benz, lenye gharama ya mamilioni ambalo limenunuliwa na rafiki zake wa karibu.

Kulingana na mrembo huyo, si mara yake ya kwanza kupewa zawadi ya gari, kwani mwaka jana alikabidhiwa kwa ajili ya kumpongeza.





## Oputa hongera baba kuijaza dunia

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Charles Oputa maarufu kwa jina la 'Charly Boy' ameshereheka kutimiza miaka 70, huku akifurahia kuwa na familia kubwa.

Mwimbaji huyo mkongwe ambaye amegeuka kuwa mwanaharakati, ameandika kupitia ukurasa wake wa Instagram,kuwa watoto wake wanampa faraja kwa kuongeza ukoo wake.

Katika ujumbe huo, Charly Boy, amesema hadi sasa ana watoto tisa,ambao sita kutoka kwa ndoa zake za zamani na watatu kutoka kwa mke wake Diane Oputa, ambaye anajulikana kama 'Lady D'.

## Obe pole sana, ubaguzi ni sumu

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Tunde Obe, amesimulia jinsi alivyokabiliana na ubaguzi wa rangi akiwa mtoto wakati akiishi marekani.

Nyota huyo wa muziki na muigizaji, kupitia ukutara wake wa Twitter, alisimulia jinsi mwanamke wa kizungu alivyomwachia mpwa wake kwenda kumjeruhi kwa sababu ya rangi yake nyeusi.

Katika simulizi hiyo ambayo amewasikitisha watu wengi, amesema tukio hilo lilitokea wakati mtoto huyo alipokuwa na umri wa miaka saba alipokwenda kumtembelea mwanafunzi mwenzake ambaye alikuwa mzungu.



RIPOTI MAALUM

# Lwakatare: Niling'angania shilingi ya Waziri bungeni hadi ruksa bodaboda

## ■ Spika alimkubali; zikaja sheria, kanuni
## ■ Chanzo alikerwa na kilichojiri Kagera

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

***KATI ya Jumatatu hadi Jumatano wiki hii, ilikuwa na sehemu tatu za makala hii kuhusu safari ya kisiasa ya Mbunge wa Bukoba Mjini, Wifred Lwakatare. Endelea na sehemu yake ya mwisho ya mazungumzo hayo.***

UNAJUA asili ya neno 'bodaboda'? Unajua kwamba liliwahi kusababisha shilingi ya Waziri kushikwa bungeni na kulitokea nini?

Mwanasiasa mwandamizi na Mbunge wa Bukoba Mjini anayestaafu, Wilfred Lwakatare, anasimulia chimbuko la usafiri huo wa pikipiki nchini 'unaobeba' ajira ya vijana wengi leo hii, ulivyosababisha mvutano mkali bungeni.

Faragha ya Nipashe na mwanasiasa huyo aliyewahi kuwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, anasimulia alivyoongoza hoja kuishinikiza serikali kufuta kodi ya kichwa.

Lwakatare, Naibu Katibu Mkuu wa zamani wa Chama cha Wananchi (CUF), pia ana simulizi ya kinachomng'oa kutoka aliko sasa, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kurejea 'nyumbani' CUF. Fuatilia maelezo yake, kutoka maswali ya 'Ana kwa Ana.'

***SWALI: Kipi cha kihistoria unadhani kinabaki kumbukumbu kwako, bungeni na nje ya ubunge?***

**LWAKATARE:** Ni mengi mno yanayobaki kama historia na nitajitahidi kutaja machache. Kumbuka nimekuwa mbunge vipindi viwili; kile cha 2000 hadi 2005 na 2015 hadi 2020. Kipindi cha 2000 hadi 2005 ninakiona kama kipindi nilichoacha kumbukumbu kubwa zaidi.

Kwanza, nikiwa bungeni nilijenga hoja ya kuhakikisha matumizi ya pikipiki kuruhusiwa kuanza kubeba abiria kibiashara.

Ikumbukwe kwamba kabla ubebaji abiria kwa pikipiki haukuwapo kabisa, bali utaratibu huo ulikuwa zaidi nchini Uganda na mpakani mwa Kenya na Uganda.

Kwenye mpaka wa Tanzania na Uganda (Mutukula), usafiri huu wa pikipiki ulikuwa zaidi ukiwavusha wafanyabiashara wa magendo ya bidhaa mbalimbali kati ya mpaka wa Tanzania na Uganda, kutoka pande zote mbili.

Hivyo, kwa kuwa usafiri huu uliwasafirisha abiria wao toka upande mmoja wa nchi na kuvuka kwenda upande wa nchi nyingine, usafiri huo wa pikipiki



Wlfred Lwakatare, alipokuwa bungeni.

ukapewa jina la bodaboda.

Jina hilo limekuwa maarufu na kutumika hivyo hivyo hata kwa maeneo yasiyo na mpaka kati ya nchi na nchi. Imechukuliwa kama jina linaloakisi usafiri wa kukodi pikipiki.

Biashara hii ya usafiri wa pikipiki ilichangamkiwa sana na vijana wa upande wa Tanzania pale Mutukula na kwa kasi wakaingiza aina hiyo ya usafiri wa pikipiki kibiashara, mpaka mjini Bukoba ambako ni jimbo langu nilililokuwa nikiliwakilisha bungeni.

Biashara hiyo ilikumbwa na tatizo la kuzuiliwa na vyombo vya dola (polisi) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kutokuwapo sheria ya kuruhusu pikipiki kubeba abiria kibiashara, pia malalamiko makubwa ya wafanyabiashara wa Taxi ambao waliona wameingiliwa kibiashara.

Vijana wengi waliojitosa katika biashara hiyo ya bodaboda, walipigwa na polisi barabarani, kuumizwa na kuangushwa barabarani na kuumia vibaya sana kwa kufukuzwa na 'defender' za polisi.

Wengi walinyang'anywa pikipiki zao na kurundikwa kwa mamia Kituo cha Polisi Bukoba. Hospitali ya Mkoa Kagera kuna wodi ilijaa vijana walioumizwa au kuvunjika au kuumizwa viungo vyao kwa kuanguka na pikipiki zao, pindi walipokuwa wakifukuzana barabarani.

Kama mbunge, niliona kuna haja kuingilia kati jambo hilo. Kwanza, pamoja na vurugu zote hizo, vijana hawakutaka kuiacha biashara hiyo, kwani ilikuwa ikiwaingizia kipato.

Hata walipokuwa wakinyang'anywa pikipiki hizo, haraka sana walikuwa wakiingiza pikipiki nyingine kutoka Uganda (zikijulikana kama bomba mbili).

Usafiri huo ulionekana kupendwa na kuwavutia watu wengi, kwa kuwa ulikuwa wa bei rahisi na uliweza kuwafikisha abiria mpaka mlangoni mwa makazi yao.

Niliwasilisha hoja bungeni nikiambatanisha na picha nyingi za majeruhi hospitalini na rundo la pikipiki kituo cha polisi. Kwa kuwa kilikuwa kipindi cha bajeti, nikaishikilia shilingi ya mshahara wa Waziri wa Mambo ya Ndani (wakati huo akiwa Omari Mapuri).

Nikaitaka serikali itoe maelezo juu ya unyanyasaji huo wa raia, pia kuitaka kuleta marekebisho ya sheria na kanuni juu ya vyombo vya kubeba abiria barabarani, pia Sheria za Usalama Barabarani.

Nimshukuru Spika (Pius) Msekwa alikuwa 'very much concerned' (aliguswa) na hoja yangu na kiti chake kikaungana nami kuibana serikali juu ya hoja hiyo.

Bila ajizi, wizara husika ikiwamo ile ya Mawasiliano na Uchukuzi iliyokuwa ikiongozwa na Profesa (Mark) Mwandosya na ya Mambo ya Ndani ya Mheshimiwa Mapuri, wakakubali kwenda kukaa na kufanya marekebisho ya sheria na kanuni.

Huo ukawa mwanzo wa mfumuko wa uingizwaji nchini maelfu ya kontena za pikipiki kutoka China na biashara ya usafiri wa pikipiki ikashamiri nchi nzima, vijijini, vitongojini na mitaani.

Hoja yangu moja tu ikatoa fursa ya kimapato kwa mamilioni ya watu; China hadi Tanzania. Ndani ya Bunge, ilifikia mahali kila nikisimama kuchangia hoja yoyote ninaitwa 'Mheshimiwa wa Bodaboda.' Ni muda wako wa kuchangia au kuuliza swali.

Ukweli ninajivunia kitu hiki hadi leo. Nikiona vijana nchi nzima wakikata mitaa barabarani wakisaka riziki wao wanasema 'kula vichwa', bila bugudha ninajisikia fahari na furaha kubwa.

Pii, nikiwa mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, nilianzisha na kuisimamia hoja iliyokuwa ikizungumzwa kwa nguvu kubwa na Mwenyekiti wa CUF, Profesa Ibrahim Lipumba, ya ufutaji suala la kodi ya kichwa iliyokuwa ikiwadhalilisha watu wengi.

Ndani ya kamati, niliijengea hoja na kusababisha serikali kwenda kujipanga upya na matokeo yake wakakubali na kwenda kuvirekebisha vitabu vyote vilivyokuwa tayari vimechapishwa. Kwa anayebisha, aende kwenye nyaraka zinazowekwa kama kumbukumbu, atalishuhudia jambo hilo!

Tatu; nikiwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (KUB), nikiongoza vyama vitano; CUF, Chadema, TLP, UDP, NCCR- Mageuzi kwa kushirikiana na baraza langu kivuli lililokuwa likiundwa na wabunge mahiri kutoka vyama vyote (Dk. Slaa, John Cheyo, Hamad Rashid, Marehemu Philemon Ndesamburo, Freeman Mbowe), tulitengeneza kanuni na kukubaliwa na wabunge wote wa upinzani na zikanisaidia kuiongoza kambi kwa umahiri mkubwa na utulivu.




Bodaboda, zikiwa eneo ambako hoja ya mbunge Wilfred Lwakatare, kuzitetea ilianzia. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

COVID-19

# Unyanyapaa ni `kifo' upo hospitalini, jamii, nyumbani

**Na Mwandishi Wetu**



USIKU wa kuamkia Aprili 19, 2020 umeandika historia katika maisha ya Hemed Mwanansali (pichani), mwalimu wa Shule ya Msingi Tandahimba mkoani Mtwara, kwani ndiyo siku alipoanza kuziona dalili za maambukizo ya corona zilizoanza kwa maumivu makali ya kichwa na taya la kulia.

Anapata dalili hizo siku 15 baada ya kurejea Tandahimba akitokea Dar es Salaam na kwamba aliondoka Dar Aprili 4, 2020 baada ya kukamilisha mambo aliyokuwa anayafuatilia. Leo Mwanansali aliyeathirika na COVID -19 ameshapona na kujiunga na familia yake baada ya kutengwa nao kwa siku 21 za kuwekwa karantini.

Akizungumza na gazeti hili hivi karibuni wilayani humo, Mwanansali anasema kuumwa corona ni tatizo kubwa lakini kilichomtesa zaidi ni kupambana na unyanyapaa kuliko hata ugonjwa wenyewe.

"Nilipata tatizo hili usiku wa kuamkia Aprili 19. Kihistoria nina matatizo ya kiafya yaliyonipata miaka minne iliyopita ninaumwa kichwa na taya la kulia, halafu maumivu yakiisha sikio la kulia linatoa maji ," anasimulia Mwanansali.

Anasema ugonjwa huo humpata kila baada ya mwezi mmoja au mitatu na kwamba anajitibu kwa dawa za miti kwa kuchemsha na kunywa maji ya maganda ya mbuyu na mlonge.

**ALIVYOPATA CORONA**

Akieleza jinsi alivyokutwa na maambukizo Mwanansali anasema usiku wa kuamkia Aprili 19 alipata maumivu makali ya kichwa na taya na kudhani ni ugonjwa unaomsumbua mara kwa mara.

"Maumivu hayakuisha hadi asubuhi, Niliamua kwenda hospitali kupimwa.Nilipofika hospitali pale getini wameweka utaratibu wa kupima joto la mwili. Nilipimwa na kukutwa na nyuzi 36.5 ambalo ni joto la kawaida. Kisha nikaenda kumwona daktari, nikamweleza ninavyojisikia na nikaomba kupima malaria.

"Lakini daktari alishtuka akasema mbona ni dalili za corona? Ghafla nikamwona daktari amepata mshtuko na kunipa barakoa nivae. Aliniuliza kama nilisafiri siku za karibuni. Nikamjibu nimerudi kutoka Dar es Salaam tangu Aprili 4 ambao ni muda mrefu," anasema.

Anasimulia kuwa daktari alikwenda kushauriana na wenzake kuhusu hali yake na ghafla kukawa na taharuki hospitalini hapo ambapo madaktari walifanya vikao kumjadili.

"Nilitarajia madaktari na wahudumu wa afya wangenitia moyo, lakini mimi ndiyo nilikuwa nawatia moyo kwani walikuwa kwenye taharuki. Nilishtukia habari zangu zimeanza kuenea hospitali hapo na mitaani. Baadhi ya madaktari hawa walinishangaza kutangaza habari za mgonjwa," anasema.

Anasema wakati muda unazidi kwenda alikuwa akitafakari endapo atapimwa na kukutwa na maambukizo ya COVID-19 itakuwaje, kwani ni mwalimu maarufu aliyefundisha shule kadhaa wilayani humo. Baada ya kuwaomba madaktari hao kumpima malaria kushindikana, anawaambia wafanye wanachotaka.

**KUTENGWA**

"Walinitenga kwenye chumba maalum, wakati wanaendelea na maandalizi mengine, hata hivyo sikupewa huduma yoyote tangu nilipofika saa 2 asubuhi. Nilikuja kuhudumiwa saa 10 alasiri kwa kupimwa malaria. Majibu yalionyesha kuwa sikuwa na malaria. Hata hivyo nilikuwa na njaa kwani sikula tangu asubuhi."

Mwalimu huyo anasema tangu wakati huo alitengwa kwenye chumba chake akisubiri kupimwa corona.

"Siku iliyofuata nilichukuliwa kipimo cha corona. Baada ya siku kadhaa majibu yalikuja. Kabla hata sijapewa majibu hayo nikasikia fununu kutoka kwa rafiki zangu kuwa majibu yanaonekana nina maambukizo. Kweli daktari alikuja siku hiyo na kuniambia nimekutwa na virusi," anasema Mwanansali.

Baada ya hapo anasema alihamishiwa kwenye kituo cha karantini kilichopo mji wa Nanyamba kilometa 10 kutoka Tandahimba na akaendelea kutumia dawa za miti kwa kunywa mara tatu kwa siku, lakini hakupewa dawa yoyote kutoka hospitalini.

"Nilikaa kwa siku 21 kwenye karantini na hali yangu iliendelea kuimarika. Madaktari walikuja kunitembelea na wakati mwingine ilikuwa mpaka niwaite. Muda mwingi nilikuwa nikifanya mazoezi," anasema walimu huyo.

**UNYANYAPAA**

Mwalimu Mwanansali anasimulia alichoakutana nacho wakati wa kuumwa kilimuumiza, kukithiri kwa unyanyapaa tangu kwa wahudumu wa afya na jamii nzima. Pia anasema awali hakukuwa na maandalizi ya kutosha kuhudumia wagonjwa hadi alipobainika.

Akielezea zaidi anasema hakukuwa na maandalizi na aliyoyaona katika kipindi chote hicho, yalifanywa baada kushukiwa kuwa ana ugonjwa huo.

"Hakukuwa na maandalizi ya kutosha hadi mimi nabainika kuwa na maambukizo. Waliandaa chumba nikiwa pale, walikuwa wakifyeka eneo na maandalizi mengine, ndiyo maana nilichelewa kuhudumiwa tangu asubuhi nilipofika hadi jioni," anasema mwalimu huyo.

> **"Nilichojifunza ni kwamba, nilipambana na unyanyapaa zaidi kuliko corona yenyewe. Unyanyapaa kutoka kwa wahudumu wa afya na jamii kwa jumla. Kwa mfano mke wa rafiki yangu aliposikia nimeambukizwa corona alimuuliza mumuwe kwa nini anakuwa na urafiki na mimi. Nilichojifunza ni kuishinda hofu ambayo ndiyo tatizo kubwa linalowasumbua wengi," anaongeza.**

"Nilichojifunza ni kwamba, nilipambana na unyanyapaa zaidi kuliko corona yenyewe. Unyanyapaa kutoka kwa wahudumu wa afya na jamii kwa jumla. Kwa mfano mke wa rafiki yangu aliposikia nimeambukizwa corona alimuuliza mumuwe kwa nini anakuwa na urafiki na mimi. Nilichojifunza ni kuishinda hofu ambayo ndiyo tatizo kubwa linalowasumbua wengi," anaongeza.

Aidha, anashauri wahudumu wa afya wapewe mafunzo ya kutosha ili wapunguze unyanyapaa kwa wagonjwa.

"Wahudumu wa afya wanapaswa kupewa ushauri wa jinsi ya kuwahudumia wagonjwa wa corona na kuwatia moyo kuliko kuwanyanyapaa. Mimi ni mgonjwa wa kwanza hapa Tandahimba, lakini inavyoonekana hakutakuwa na mwingine kwa sababu watu wanaogopa unyanyapaa. mtu atakohoa atajitibu mwenyewe huko huko kuliko kwenda hospitali," anaeeleza.

**MAONI YA VIONGOZI**

Hata hivyo, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tandahimba, Athumani Suleiman, anakanusha kuwapo kwa unyanyapaa katika hospitali ya hiyo akisema kilichotokea ni hali ya taharuki tu.

"Si kweli kwamba mgonjwa alinyanyapaliwa, kwa sababu alipokwenda pale alipokelewa kama mgonjwa wa kawaida. Kwa kuwa huu ugonjwa ni mpya kulikuwa hali ya taharuki na kumekuwa na hofu kiasi kwamba hata mtu akikohoa watu wanadhani ni corona," anasema Suleiman.

Akizungumzia juhudi zilizochukuliwa na Halmashauri hiyo kupambana na ugonjwa huo, Sulaiman amesema wilaya hiyo ilifanya maandalizi mapema ikiwa pamoja na kuunda kamati ya kuratibu ugonjwa huo na vituo vilivyoandaliwa kwa ajili ya kupokelea wagonjwa.

"Tulianzisha kamati kwa mujibu wa mwongozo wa Wizara ya Afya na tunakutana kila Jumatano kutathmini hali ya maambukizo ilivyo. Kamati hiyo inahusisha madiwani, viongozi wa dini na wa kata," anasema Suleiman.

Anaongeza kuwa halmashauri hiyo imetumia mapato yake ya ndani kununua vifaa vya kuwakinga na maambukizo wahudumu wa afya na wagonjwa wanaofika katika hospitali na vituo vya afya.

HABARI KIMATAIFA

# Baraza la mawaziri kuitawala Burundi hadi rais mteule atakapoapishwa

**BUJUMBURA, Burundi**

BARAZA la Mawaziri nchini Burundi, limesema linaongoza nchi hiyo hadi Rais mpya atakapoapishwa mwezi Agosti.

Uamuzi huo ulifikiwa kufuatia mkutano uliofanywa siku ya Alhamisi chini ya uongozi wa Makamu wa Rais wa kwanza, Gaston Sindimwo.

Tangu kutokea kifo cha ghafla cha Rais Pierre Nkurunziza, hadi sasa bado haijajulikana lini kiongozi mpya ataapishwa.

Katiba ya nchi hiyo imeweka wazi kuwa Spika wa bunge Pascal Nyabenda, alitakiwa kushikilia wadhifa huo katika kipindi cha mpito hadi hapo Jenerali Évariste Ndayishimiye, ambaye ni mshindi wa nafasi hiyo kupitia chama cha CNDD-FDD katika uchaguzi uliofanyika Mei 20 atakapoapishwa.

Taarifa ambazo hazijathibitishwa zinasema, Jenerall Ndayishimiye, pia ni mgonjwa.

Tovuti ya kibinafsi pamoja na vyombo vingine vya habari, vilisema kuwa mawaziri waliifahamisha mahakama ya Katiba, kuhusu uamuzi huo.

Mahakama hiyo inasubiriwa kutoa uamuzi ni nani anastahili kuapishwa kuwa rais, ilisema taarifa iliyochapishwa na tovuti ya Iwacu.

Rais wa zamani, Sylvestre Ntibantunganya, ametoa wito kwa Ndayishimiye aapishwe mara moja kama rais wa Burundi.

***BBC***




Sanamu ya Rais wa zamani wa Marekani, Jefferson Davis, ikiwa imelala barabarani baada ya waandamanaji wa mjini Richmond, Virginia kuiangusha chini katika maandamano ya kupinga mauaji ya George Floyd yanayoendelea.Sanamu hiyo imekuwa alama ya Jimbo hilo kumkumbuka kwa kuimarisha biashara ya utumwa **(PICHA:AFP)**

# Trump awawekea vikwazo watumishi ICC

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ameidhinisha vikwazo vya kiuchumi na usafiri dhidi ya watumishi wa mahakama ya kimataifa ya uhalifu, ICC, waliochunguza wanajeshi wa Marekani waliofanya uhalifu wa kivita nchini Afghanistan.

Maofisa wa serikali ya Trump, wamesema mahakama hiyo yenye makao yake mjini The Hague, inatishia kuingilia uhuru wa ndani wa Marekani.

Pia waliituhumu Urusi kwa kuidanganya ili kuyafanyia kazi maslahi yake. Umoja wa Mataifa kupitia msemaji wake Stephane Dujarric, ulielezea wasiwasi wake kuhusu hatua hiyo.

Mahakama hiyo ya Kimataifa kwenye taarifa yake imesema kwamba, hatua hiyo ilikuwa ya karibu katika mfululizo wa mashambulizi dhidi yake.

Imesema mashambulizi hayo ni uchochezi na jaribio lisilokubalika la kuingilia utawala wa sheria na michakato ya kisheria ya mahakama hiyo.

***DW***

# UAE yaionya Israel kunyakua Ukingo wa Magharibi

**WASHINGTON, Marekani**

BALOZI wa Umoja wa Falme za Kiarabu nchini Marekani, ameionya Israel kuwa haitakuwa na uhusiano wa kawaida na mataifa ya Kiarabu, endapo itanyakua ardhi katika maeneo ya Ukingo wa Magharibi.

Baadhi ya maofisa wa Israel wamepuuza maoni kuwa hatua ya kujitanua kwa Israel kwenye makazi ya kilowezi katika bonde la Jordan katika Ukingo wa Magharibi, itaathiri mchakato wa chini chini wa kuimarisha uhusiano kati yake na nchi za Kiarabu.

Balozi huyo, Youssef Al Otaiba, alisema hatua hiyo itachochea vurugu kutokana na unyakuaji huo usio halali wa ardhi ambayo Wapalestina wanaitambua kama sehemu ya taifa lao.

**DW**

**el wamepuuza maoni kuwa hatua ya kujitanua kwa Israel kwenye makazi ya kilowezi katika bonde la Jordan katika Ukingo wa Magharibi, itaathiri mchakato wa chini chini wa kuimarisha uhusiano kati yake na nchi za Kiarabu.**

# Waziri Mkuu awalipa majambazi mil-55.6 kumuua mkewe

**MASERU, Lethoto**

ALIYEKUWA Waziri Mkuu wa Lesotho, Thomas Thabane, imedaiwa aliwakodi watu na kuwalipa pesa kwa ajili ya kumuua mke wake wa kwanza.

Taarifa iliyotolewa na polisi wa chi hiyo, inaeleza kazi hiyo iliratibiwa na mke wa sasa wa kiongozi huyo, Maesaiah, ambaye aliwalipa fedha majambazi na kutekeleza mauaji hayo mwaka 2017.

Lipolelo Thabane ambaye ni mke wa zamani wa Thabane, alipigwa risasi na kuuawa usiku wa kuamkia siku ya kuapishwa kwa waziri mkuu huyo.

Polisi katika moja ya stakabadhi zilizowasilishwa mbele ya Mahakama Kuu ya mjini Maseru, inapinga ombi la mke wa Thabane, ambaye amekamatwa aachiliwe kwa dhamana.

Maesauah amewekwa rumande tangu wiki iliyopita akiwa anakabiliwa na mashtaka ya mauaji,

Hata hivyo, jopo la mawakili wanaomtetea wanataka aachiliwe kwa dhamana ili akamhudumie mumewe ambaye ni mgonjwa.

Thabane alilazimika kujiuzulu nafasi yake ya waziri mkuu kutokana na madai hayo ya mauaji. Hata hivyo anakana kuhusika na tukio hilo.

Mpaka sasa bado hajafunguliwa mashitaka rasmi, lakini stakabadhi za polisi zinadai kuwa aliwaonyesha majambazi nyumbani kwa mke wake wa zamani ili kutekeleza mpango huo.

Polisi pia wanasema waziri mkuu huyo wa zamani na mke wake walidaiwa kuwalipa majambazi paundi za Uingereza, 142,000, sawa na Sh. milioni 416.8.

Watu hao walilipwa kiasi cha milioni 55.6 kama malipo ya awali, kwa mujibu wa stakabadhi hizo zilizowasilishwa mahakamani chini ya kiapo.

Mmoja wa watu waliohusika katika mauaji hayo anatarajiwa kutoa ushahidi wake.

Lipolelo Thabane alipigwa risasi akiwa kando ya barabara wakati akirudi nyumbani akitoka katika kijiji kidogo kilichopo nje ya mji mkuu.

Katika maisha yake ya ndoa, alipewa talaka kutokana na maisha yao kutawaliwa na migogoro, hasa baada ya Thabane alipoamua kuishi na Maesaiah, mwenye umri wa miaka 42 kama mkewe.

Kabla ya kuapishwa nafasi ya waziri mkuu, Lipolelo alishinda kesi ya kutambuliwa kama mke wa kwanza wa kiongozi huyo.

***BBC***

# HADITHI


ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

# Mauaji Harusini-16

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**




Alisikia simu yake ikiiita. Alichukua na kuangalia jina. Moyo ulimshtuka kwa mbali.

"Shani." Alitamka na mwenyewe hakujua kama alikuwa akisema au kuuliza.

"Halo mrembo vipi mambo?" Haraka haraka alianza kumuuliza, kabla hajasalimiwa.

Alijiona kama vile nafsi inamsuta. Ni yeye ndiye aliyepigiwa simu badala ya yeye kupiga.

Hata hivyo alijipa moyo na kujiambia "Haiwezekani nionekane nimekuwa dhaifu na binti mdogo kama huyu."

"Hata kunitafuta ndugu yangu?" Sauti ya Shani ilisikika upande wa pili.

"Hapana, unajua nisingeweza kukutafuta haraka haraka tu, nilitaka nikutafute wakati nimetulia na wewe pia umetulia." Alijibu na kutabasamu, kwani aliona jibu hilo ni muafaka.

"Kweli eee?"

"Ni kweli binamu yangu."

Eddy alisikia kicheko kikali kutoka kwa Shani.

"Mbona umefurahi sana?"

"Nimefurahi kusikia unaniita binamu yangu."

"Kwani uongo? Baba yako mzazi Patiyo si alimuoa shangazi yangu, sasa kwa nini usiwe binamu yangu?"

"Binamu gani? Au binamu kinyama cha hamu."

"Vyovyote vile."

Jibu hilo la Eddy lilimfanya Shani kuangua kicheko kikali kuliko cha mwanzo.

"Binamu leo umeamka na vicheko, tofauti na siku ile kule makaburini."

"Unanifurahisha, kumbe una maneno hivyo. Wala sikujua hilo." Shani alisema huku akikohoa kikohozi chepesi

"Nataka siku uje nyumbani hapa, naona kutachangamka kweli, maana kwa muda mfupi tu nimegundua kuwa wewe ni mchangamfu sana."

"Unafikiri mchamgamfu basi, sema basi tu. Ila hilo la kuja nyumbani kwako naliafiki kwa sababu nataka kuja kukuona ukiwa nyumbani. Nikuone ukipika."

Bado Shani alikauka na kucheka.

"Unataka ukija nikupikie nini?"

"Ugali, dagaa na mchicha."

Jibu hilo pia lilikuwa kama kichekesho kwa Shani.

Kwa mbali Shani alianza kuamini kile kitu ambacho alichokuwa akiwaza usiku kucha.

Tangu alipotoka makaburini, alikuwa akimuwaza Eddy. Hakujua ni kwa nini akili yake ilikuwa kwa mtu yule.

"Anaonekana ni mtu spesheli sana." Aliwaza akiwa kitandani.

Alikumbuka jinsi alimvyomshika na kumkumbatia kwa huruma na upendo. Maneno yake ya faraja, kutia moyo, lakini ya kujiamini pia alimshangaza na kumfurahisha mno Shani

"Pole Shani, najua jinsi unavyoumia kwa kumkosa baba yako kutokana na baadhi ya watu wenye roho mbaya.

Nakuahidi, watu wote waliofanya mauaji haya, na yoyote aliye nyuma ya mpango huu, ni lazima watapatikana na kulipa maovu yote haya."

Akakumbuka maneno ya kijasiri yaliyotoka kwenye kinywa cha kijana yule.

"Usilie. Msichana mdogo, mzuri na mrembo kama wewe hupaswi kulia hapa. Angalia watu waliopita njiani wanakuangalia unavyolia. Mimi mwenyewe nimeumia kutokana na kifo cha shangazi yangu, lakini silii. Mungu anasema umuombe huku na wewe unafanya kazi. Kazi itakayofuata sasa ni kuwasaka wauaji."

Akakumbuka maneno mengine ambayo Shani aliona kabisa kuwa yule jamaa aliyekutana naye hakuwa wa kawaida.

"Ana maneno ya kijasiri, lakini ana maneno ya faraja na upendo" Alijisemea.

Ghafla tu Shani alianza kupenda staili ya kijana yule "Sipaswi kumuacha. Kwa sasa natarajiwa kuabidhiwa mali za baba yangu. Mimi bado ni msichana mdogo. Huyu kuna kitu anaweza kunisaidia. Anaweza kuwa mshauri mzuri kwangu." Alijisemea mwenyewe, ukiwa tayari ni usiku wa manane lakini alikuwa bado hajapata lepe la usingizi.

Kumuwaza Eddy ndiko kulikofanya ampigie simu haraka tofauti na mwenyewe alipovyofikiria.

"Mimi nataka nikupikie pilau." Shani alimjibu baada ya kumaliza kicheko chake.

"Hapana mrembo, mimi pilau huwa nakula siku za sikukuu tu."

Shani alijizuia kucheka tena, lakini hakuweza.

"Haya baba, nitakupikia, ufurahi."

"Usisahau nyanya chungu."

Maneno ya Eddy, yenye mchanganyiko ya ucheshi na mzaha yalimfanya Shani kuzidi kuhitaji kuwa na mtu wa aina hiyo.

**"Usilie. Msichana mdogo, mzuri na mrembo kama wewe hupaswi kulia hapa. Angalia watu waliopita njiani wanakuangalia unavyolia. Mimi mwenyewe nimeumia kutokana na kifo cha shangazi yangu, lakini silii. Mungu anasema umuombe huku na wewe unafanya kazi. Kazi itakayofuata sasa ni kuwasaka wauaji."**

Alizaliwa mtoto wa pekee, tena kwenye familia ya kitajiri. Mara nyingi alikuwa peke yake. Faraja pekee aliipata akiwa shule akiwa anacheza na rafiki zake. Lakini nayo walikuwa ni watoto wa kitajiri, hivyo wengi walikuwa ni wajivuni. Hakuwa wachangamfu na wacheshi. Kwa muda mrefu Shani aliishi kipweke. Na aliizoea hali ile. Aliiona ya kawaida.

Tangu alipokutana na Eddy na maneno yake, kuna kitu ambacho alihitaji kutoka kwake. Alihitaji kuwa naye angalau masaa mawili ili aangalie kuna nini ndani yake.

"Sawa, sasa utakuja lini?"

"Kwanza hujaniambia unaishi wapi?"

"Kwa sasa nipo Mbweni."

"Kwa baadaye utakuwa wapi?"

Swali hilo lilimtatiza na kuchekesha Shani na kujiona ni kama alijibu vibaya.

"Baba yangu ana nyumba nyingi hapa mjini. Kuna wakati nakuwa nipo Kigamboni, kwenye nyumba mpya ambayo ndiyo aliyokuwa anakwenda kuishi na mkewe, lakini kuna nyumba yetu nyingine Kigamboni. Huku ndiyo nimechagua nikae mimi kwa sasa. Siwezi kukaa Kigamboni kutokana na lile tukio lililotokea." Alijibu kwa unyeyekevu.

"Nimekuelewa. Leo si Ijumaa? Nitakuja Ijumaa ijayo?"

"Mbona mbali hiyo jamani?" Shani alilalamika.

"Najua. Lakini vumilia tu. Mambo mazuri hayataki haraka."

Shani alikubaliana na Eddy na kukata simu. Akaibusu.

"Mambo mazuri gani tena hayo." Alijisemea mwenyewe baada ya kukata simu.

Kwa mara ya kwanza Shani alijiona kwenye furaha zaidi kuliko wakati mwingine wowote ule.

Aliwaza jinsi atakavyotembelewa na mwanaume jasiri, mwenye kujiamini, mchangamfu na mcheshi kwa jinsi tu alivyomuona.

"Itakuwa ni siku ya furaha sana." Alisema kwa sauti. Lakini ndani alikuwa peke yake. Wafanyakazi wake wawili, wa kike na wa kiume walikuwa nje wakiendelea na shughuli zao.

***Itaendelea Jumamosi***

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA KAZI**

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUCAS S.MWEGO** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 485 AER** aina yake **PEUGEOT.** Kwa yeyote atakeiona anaombwa atoe taarifa ktk kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MOR/MOR/RB/440116/2020.**

115772702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI -TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi NAMBA 78/2020**

**Ombi la REHEMA NG'ANZI CHOYO kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu NG'ANZI JUMAA**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 15/6/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Sahihi ya Hakimu

115772902

## KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI

**EMILLIAN ENGEREBERT MABOKO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI ZENYE NAMBA ZA USAJILI **T605 CBJ** AINA YA NISSAN PICK_UP YENYE CHASSIS NO **QGD21440443** NA ENGINE NO **NA20C5179**

TAARIFA YA POLISI **KAH/RB/211/2020**

NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 977DKF** AINA YA MITSUBISH CANTER YENYE CHASSIS NO **FE648F520856** NA ENGINE NO **Z549HQ**

KWA YOYOTE ATAKAZIEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

TAARIFA YA POLISI
**KAH/TR/RB/211/2020**

115773002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**

**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;147/2020**

**Ombi la JOSEPHA DAMIAN CHUVAKA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu GERALD JOHN MARK**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 06/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 10/06/2020.

Tarehe 10/6/2020

Sahihi ya Hakimu

115773102


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# WENGER:

## BARCA KUNUNUA MSHAMBULIAJI MWINGINE

**BARCELONA, Hispania**

ARSENE Wenger "anashawishika" Barcelona watasajili mshambuliaji mwingine licha ya kutarajia kuimarika kwa, Antoine Griezmann.

Griezmann amekuwa akikabiliwa na wakati mgumu kurudi kwenye kiwango chake katika msimu wake wa kwanza pale Barca, akifunga mabao 14 kwenye mechi 37 tangu alipotua pale kwa ada ya euro milioni 120 akitokea Atletico Madrid.

Barca wamekuwa wakihusishwa sana na nyota wa Inter Milan, Lautaro Martinez, ambaye anafikiriwa kama mrithi wa muda mrefu wa Luis Suarez.

Kocha wa zamani wa Arsenal, Wenger anaamini Griezmann ataimarika, lakini anahisi Barcelona wataongeza fowadi mwingine mwishoni mwa msimu.

"Barcelona mara zote wamekuwa wakinunua wachezaji wakubwa. Binafsi sina uhakika kama Suarez anahitaji mrithi wake," amesema akiiambia beIN SPORTS.

"Wanaweza kuongeza mshambuliaji mwingine kwa sababu ni kweli kwamba, Suarez na (Lionel) Messi ndio wenye mchango mkubwa zaidi na watahitaji mtu mwingine anayeweza kufunga mabao.

"Bado nafikiri Griezmann kwa hatua fulani ataanza kufunga mabao, anaonekana bado hajazoea kabisa mfumo, labda sasa ataanza kufunga kwa sababu yeye ni mfungaji mzuri sana.

"Lakini nashawishika watanunua mshambuliaji mwingine."



# LAMPARD

## AWAFUNGIA KAZI WERNER, KAI

**LONDON, England**

FRANK Lampard amepanga kufanya marekebisho makubwa kwenye kikosi cha Chelsea kwa kuleta nyota wengi zaidi wakati dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa, kwa mujibu wa Daily Mail.

Inadaiwa Chelsea wamekubaliana na RB Leipzig kumsajili, Timo Werner kwa pauni milioni 53.8, dirisha litakapofunguliwa na wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kumwania, Jadon Sancho na Kai Havertz.

Hata hivyo, kwa sasa imemwondoa Sancho kwenye orodha ya wachezaji inaowataka kuwasajili kwenye dirisha lijalo, kwa sababu wamepata uhakika wa asilimia 100 nyota huyo wa England atakwenda kujiunga na Manchester United.

Lakini sasa Lampard yupo kwenye mbio za kuwania saini ya nyota wa Bayer Leverkusen, Havertz wakiamini watakuwa wamepata mchezaji mwenye ubora kama ule ule wa Sancho.

United wanatajwa pia kumtaka Havertz na wanapewa nafasi kubwa ya kukamilisha dili hilo, licha ya Lampard kusema kwa staa huyo wa Ujerumani wana uhakika wa kumpata.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, amefunga mabao matano katika mechi nne alizocheza tangu Bundesliga iliporejea kutokana na janga la virusi vya corona.



# Makali ya Salah yamshangaza Mikel

**LONDON, England**

JOHN Obi Mikel amesema anashangazwa na namna Mohamed Salah alivyoibuka na kucheza soka la kiwango cha juu kwa sasa, wakati miaka michache iliyopita, alikuwa mchezaji wa kawaida sana.

Wachezaji hao wawili walikuwa pamoja pale Chelsea, ambapo Mo Salah hakuweza kutamba, akiishia kucheza mechi 13 tu kwenye Ligi Kuu England na kutolewa kwa mkopo kwenda Fiorentina.

Kisha alitolewa tena kwa mkopo AS Roma, kabla ya kuuzwa jumla katika timu hiyo ya Serie A.

Lakini, mwaka 2017, alirudi kwenye Ligi Kuu England akinaswa na Liverpool na tangu hapo amekuwa mmoja wa washambuliaji bora kabisa duniani, akibeba kiatu cha Dhahabu cha England kwa misimu miwili mfululizo, huku akifunga mabao 91 katika mechi 144 za michuano yote aliyochezea miamba hiyo ya Anfield.

"Salah alipokuja Chelsea, alikuwa kijana mdogo, alikuwa mtulivu sana na kila mtu alimpenda," amesema akinukuliwa na Sky Sport.

"Sikuwahi kufikiria kabisa angefikia kiwango hiki alichonacho kwa sasa, naona maajabu makubwa kwa kweli."

Salah na kikosi chake cha Liverpool kitarejea kumalizia Ligi Kuu wiki ijayo watakapopambana kuwania taji lao la kwanza la Ligi Kuu England ambalo wamesubiri kwa miaka 30.



# SAHA

## AMTAJA MBAPPE BORA KULIKO WOTE DUNIANI

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe amesifiwa kama "mchezaji wa aina yake anayezifanya klabu kubwa kumuota" wakati Paris Saint-Germain wakijaribu kumbakisha nyota huyo raia wa Ufaransa.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 21 alikuwa mchezaji wa kwanza tangu Pele mwenye umri mdogo kufunga kweye fainali ya Kombe la Dunia miaka miwili iliyopita wakati Ufaransa ikiitwaa kombe hilo nchini Urusi.

Straika wa zamani wa Ufaransa na Manchester United, Louis Saha amesema Mbappe pengine ndiye mchezaji "mwenye thamani kubwa zaidi duniani", na kudai klabu nyingine kubwa zinawania saini yake ikiwamo Real Madrid.

Mbappe alifunga mabao 33 kwenye Ligi Kuu Ufarabsa, Ligue 1, kwa msimu wa 2018-19, licha ya kuanza kwenye mechi 24 pekee, kabla ya ligi kufutwa msimu huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

"Kwa uhakika kabisa yeye ni mchezaji aliyekamilika na anajua wapi kwa kwenda," alisema Saha akiiambia Stats Perform News.

"Tayari ni mchezaji kijana kwa umri. Amepevuka sana, na anajua nini anataka. Hawezi kuficha na hilo ndio uzuri zaidi wake."

## PULIS: TRAORE USIENDE LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

KOCHA aliyemuibua nyota wa Wolves, Tony Pulis, Adama Traore, amemshauri mchezaji huyo kuachana na mpango wa kutua Liverpool wakati kipindi cha dirisha la majira haya ya joto litakapofunguliwa.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp amekuwa akihusishwa na mpango wa kumnasa staa huyo wa Wolves, Traore baada ya kuona ameshindwa kufanya kweli kwenye uhamisho wa Timo Werner, ambaye anatajwa kujiandaa kwenda Chelsea.

Pulis, ni kocha wa Traore aliyemnoa akiwa Middlesbrough kabla ya kuhamia Wolves kwa ada ya pauni milioni 18, na sasa amemwambia fowadi huyo asiende Liverpool, badala yake abakie pale Molineux. Kocha huyo anaamini kusalia hapo kutamfanya Traore apate nafasi ya kujumuishwa kwenye kikosi cha Hispania kitakachokwenda kuchuana kwenye fainali za michuano ijayo ya Euro.

Traore amekuwa kwenye kiwango bora msimu huu, akifunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho 10, huku akiwa anachezeshwa pembeni na Kocha Nuno Espirito Santo.

"Adama ana uwezo wa kucheza kila siku," amesema Pulis akinukuliwa na Sky Sport.

"Amekuwa akijiamini sana. Kwa sasa yupo chini ya kocha mwingine na amekuwa akimpa nafasi ya kucheza kila wakati. Ni rafiki yangu.

"Hata kocha wake wa sasa nadhani wamekuwa na uhusiano mzuri. Amemtengenezea mazingira ya kumfanya awe na nafasi ya kuingia kwenye kikosi cha Hispania."

## ARSENAL KUMTUMIA BABA KUMBAKIZA AUBAMEYANG

**LONDON, England**

ARSENAL sasa wameamua kumtumia baba mzazi wa Pierre-Emerick Aubameyang ili kumshawishi kusaini mkataba mpya hapo kwenye Uwanja wa Emirates, kwa mujibu wa Sky Sport

Aubameyang, amekuwa akihusishwa na klabu za Real Madrid, Barcelona na Manchester United wakati akiingia kwenye mwaka wa mwisho wa mkataba wake katika kikosi hicho cha washika bunduki.

Kutokana na hilo, Arsenal bado hawajafanya uamuzi ama wampige bei kwenye dirisha lijalo la uhamisho wa majira ya kiangazi au wabaki naye kwenye kikosi na kumpoteza bure itakapofika mwakani.

Fowadi huyo wa kimataifa wa Gabon msimu uliopita alishinda kiatu cha dhahabu cha Ligi Kuu England sambamba na nyota wa Liverpool, Sadio Mane na Mohamed Salah na msimu huu akishika namba mbili kwa wanaoongoza kwa mabao.

Arsenal wanapambana abaki wakiamini kurejea kwao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kutatoa nafasi ya mshambuliaji wao huyo kubakia Emirates.

Lakini, baadhi ya mabosi kwenye timu, wanaamini kupitia uhusiano wao mzuri na Pierre-Francois Aubameyang, ambaye ni baba wa mchezaji huyo utasaidia kumshawishi kubaki kwenye kikosi.

Wanaomsimamia Aubameyang ni ndugu zake, huku jina la baba likiwa limeonekana kwenye karatasi zilizohusu uhamisho wa mchezaji huyo alipotua Arsenal akitokea Borussia Dortmund kwa ada ya pauni milioni 56 Januari 2018.

Arsenal itarejea kwenye ligi msimu huu ikiwa inashika nafasi ya tisa kwenye msimamo watakaposafiri hadi Etihad kuwakabili Manchester City, Juni 17.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ZIDANE ATANGAZA KUMHITAJI KANTE

●●●Lengo la kumsajili Mfaransa huyo ni kuimarisha safu yake ya kiungo kuelekea msimu ujao...

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid imefufua upya mchakato wa kumsajili kiungo wa Chelsea, N'Golo Kante katika majira ya joto na imewasilisha ofa ya pauni milioni 71 ili kumnasa nyota huyo.

Klabu hiyo ya La Liga inataka kumsajili Kante ili kuimarisha safu yake ya kiungo na imekuwa ikivutiwa na nyota huyo kwa muda mrefu, tangu alipokuwa akichezea Leicester City.

Jarida la AS limeandika, Real Madrid inaamini itafanikiwa katika mchakato huo wa kumsajili Kante kwa sababu ili kujiweka imara na vile vile itaisaidia Chelsea ambayo ina mpango wa kuuza wachezaji wake kupata fedha za kutumia kwenye dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa.

Inaelezwa kuwa tayari Chelsea imeshamnasa nyota wa Ajax, Hakim Ziyech, kwa ada ya pauni milioni 36.5 na atajiunga na kikosi hicho kwenye kipindi cha majira ya joto.

Pia inaonekana kuwa The Blues iko karibu kumnasa kiungo mshambuliaji wa RB Leipzig, Timo Werner, ambaye ada yake ya uhamisho iliyotajwa kwenye mkataba wake ni pauni milioni 53.

Hata hivyo, Madrdi inayofundishwa na Zinedine Zidane, itatakiwa kulipa kiasi hicho cha ada kabla ya Jumatatu, baada ya hapo thamani ya mchezaji huyo itaongezeka.

Kikosi hicho kinachoongozwa na Frank Lampard, pia kinatajwa kuwa kwenye mchakato wa kuwania saini ya nyota wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz, ambaye pia anaichezea Timu ya Taifa ya Ujerumani na thamani yake ni pauni milioni 75.

Kama Chelsea itafanikiwa kuwasajili Werner na Havertz, inaonekana baadhi ya wachezaji wenye majina makubwa walioko katika timu hiyo wanaweza kuondoka Stamford Bridge.

Kante amekuwa na wakati mzuri katika kikosi cha Chelsea, akishinda taji la Ligi Kuu England, Kombe la FA na Ligi ya Europa.

Mkataba wa nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, umebakiza miaka mitatu katika klabu hiyo.

## KWA UFUPI

**CORONA YAMGUSA WERNER**

HATIMA ya uhamisho wa straika wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner (24), kutoka RB Leipzig kuelekea Chelsea kwa ada ya pauni milioni 52 imeshikiliwa na mtikisiko wa kiuchumi ambao umesababishwa na janga la Covid-19. ***(The Athletic -subscription required)***

**BARCA YASAKA MABEKI**

BARCELONA imeanza mchakato wa kusajili mabeki kutoka Tottenham na Chelsea ambao wataingia kwenye sehemu ya usajili wa nyota wake Mbrazil Philippe Coutinho, ambaye ana umri wa miaka 27. ***(Sport via Mail)***

**BELLERIN ANUKIA INTER**

INTER Milan inajipanga kuwasilisha ofa ya pauni milioni 27 kwa ajili ya kumsajili beki wa kulia wa Arsenal, Hector Bellerin (25), licha ya Mhispania huyo kubakiza miaka mitatu katika mkataba wake na klabu hiyo. ***(Express)***

**MULLER AMKARIBISHA KAI**

MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich, Thomas Muller, amesema anamkaribisha kiungo wa Timu ya Taifa ya Ujerumani na Bayer Leverkusen, Kai Havertz (21), ambaye anatajwa kuondoka Leverkusen ifikapo majira ya joto. ***(Metro)***

**BELLINGHAM NJIA PANDA**

MCHEZAJI nyota wa Birmingham City, Jude Bellingham (17), anaonekana anajiandaa kukacha ofa ya kujiunga na Manchester United na kukubali kuelekea kwa vigogo wa Bundesliga, Borussia Dortmund. ***(Sport Bild via Talksport)***

**TOLISSO AIKANA UNITED**

WAKALA wa kiungo wa Bayern Munich, Corentin Tolisso, amekanusha kuwa amefanya mazungumzo na Manchester United kuhusiana na uhamisho wa Mfaransa huyo ambaye ana umri wa miaka 25. ***(Standard via Sky Germany)***

**JUVE, BARCA ZATETA**

JUVENTUS na Barcelona zinaendelea na mazungumzo yanayohusisha uhamisho wa viungo Miralem Pjanic (30) na Arthur Melo ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Independent)***

**PASALIC KUIBEBA CHELSEA**

CHELSEA inajipanga kutumia pauni milioni 13.5 zitakazotokana na uhamiso wa majira ya joto baada ya kumuuza kiungo wake, Mario Pasalic kwa Atalanta ambayo alikuwa akiitumikia kwa mkopo kwa muda wa miaka miwili. ***(Football London)***

**DISASI AKARIBIA WOLVES**

WOLVES imeingia kwenye mbio za kuwania saini ya beki wa Rennes, Axel Disasi ambaye anawaniwa na klabu nyingine mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu England. Klabu hiyo imewasilisha ofa ya pauni milioni 13.5 ili kumnasa Mfaransa huyo. ***(L'Equipe - in French)***

**SPURS, DIER SAFI**

TOTTENHAM inaendelea kujiimarisha katika kukamilisha mazungumzo ya kusaini mkataba mpya na kiungo wake, Eric Dier katika majira ya joto, kabla ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 kuingia kwenye mwaka wa mwisho wa mkataba wake. ***(Football Insider)***

**LIVER YAMFUATA ZANIOLO**

LIVERPOOL inatajwa kuanza mchakato wa kumsajili kiungo wa Roma, Nicolo Zaniolo, lakini klabu hiyo ya Serie A inaonekana haiko tayari kumuuza nyota huyo mwenye umri wa miaka 20. ***(Tuttosport)***

HABARI MICHEZO

# POLISI TANZANIA YATUMA SALAMU YANGA, AZAM FC

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, amesema mikakati yake sasa ni kuona timu hiyo inamaliza katika nafasi tano za juu kwenye msimamo Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Malale alisema anakiandaa kikosi chake kuongeza nguvu na kupambana kusaka pointi zaidi katika mechi zilizobakia ili wapande juu kutoka nafasi ya sita ambayo wako sasa.

Malale alisema viwango vya wachezaji wake si vibaya na muda waliorejea kufanya mazoezi baada ya ligi kuruhusiwa kuendelea umewaimarisha na wanatarajia kupata matokeo chanya katika michezo yao tisa iliyobakia.

"Sio mbaya sana ila muda tulikaa nao wamerudi kwenye hali yao kama mwanzo, mpaka sasa sina majeruhi, nashukuru Mungu mpaka sasa kikosi kiko vizuri sana," alisema Malale.

Aliongeza kila mchezaji ana morali ya kufanya vizuri ili kufikia malengo ya timu ambayo ni kutopoteza pointi kwenye michezo yao iliyobakia kwa kumalizia msimu huu.

"Tumerejea katika ligi, tutaanza na Lipuli, tunawaheshimu wapinzani wetu sababu kila timu inajiandaa kutafuta alama muhimu ili kujiweka katika nafasi nzuri katika msimamo wakati huu ligi inapokaribia kumalizika," alisema Malale.

Aliongeza wamejipanga kusaka matokeo mazuri ili kuendelea kuwafurahisha mashabiki wao wanaowaunga mkono kwenye mechi zote wanazocheza.

"Tutakapokuwa tunashinda, tutajiweza kwenye mazingira mazuri ya kuwalinda mashabiki wetu, hatutaki kuwaangusha, tunataka kuwapa furaha kila wanapokuja kutushangilia, ushindi ndio zawadi pekee wanayostahili kuipata," Malale aliongeza.

Polisi Tanzania wataikaribisha Lipuli FC kutoka Iringa katika mchezo utakaochezwa Juni 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Chuo cha Polisi Moshi, Kilimanjaro.



Mchezaji Yasini Mohamed (kulia), akisukuma kete dhidi ya mpinzani wake, Mohamed Ndembo, katika mashindano ya Taifa ya Drafti yanayoendelea kwenye Ukumbi wa Java ulioko Kitunda jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Ndanda yaahidi 'kufia' uwanjani

Na Saada Akida

TUTAPAMBANA hadi mwisho. Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Ndanda FC ya Mtwara, Meja Mstaafu Abdul Mingange kuelekea katika hatua ya lala salama ya msimu wa 2019/20 wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mingange aliliambia gazeti hili changamoto ya majeruhi na ukata wa kifedha waliyonayo haitarudisha nyuma mipango yake ya kuinusuru timu hiyo.

Alisema wachezaji wote alionao wanaendelea kujituma kwenye mazoezi kwa sababu wanataka kuona wanaendelea kuonekana tena katika msimu ujao wa Ligi Kuu Bara.

Aliwataja wachezaji ambao ni majeruhi na atawakosa katika mechi za awali ni pamoja na Samuel John na Godfrey Malibicha.

"Tuna majeruhi katika kikosi chetu na hali mbaya ya kiuchumi imesababisha baadhi ya wachezaji wangu kutofika kambini kwa muda muafaka, lakini tunaahidi tutapambana hadi mwisho," alisema Mingange.

Alieleza anahitaji kupata pointi 12 ili kufikisha alama 42, ambazo zitamwondoa kwenye janga la kushuka daraja.

"Tupo ICU ila wadau wa soka wasiwe na wasiwasi, hatutashuka daraja, tutavuka mtihani na majaribu haya tuliyonayo," Mingange alisema.

# Kabbadi kuhamia Arusha, Mwanza

Na Shufaa Lyimo

CHAMA cha Kabbadi Tanzania kinatarajia kupeleka makocha wa mchezo huo katika mikoa mbalimbali nchini, ili kuzalisha wachezaji wapya, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa chama hicho, Abdallah Nyoni, alisema mafunzo hayo yataanza kutolewa katika mikoa ya Mbeya, Arusha na Mwanza.

Nyoni alisema wanaamini mpango huo utasaidia kupata wachezaji wazuri watakaounda kikosi cha Taifa.

Alisema wameamua kuanza na mikoa hiyo kwa sababu ya kupokea mialiko maalumu kutoka kwa wadau wa mchezo huo ambao wameahidi kugharamia malazi na chakula cha wakufunzi watakaopelekwa huko.

"Tunatamani tupeleke walimu mikoa yote ya Tanzania, isipokuwa tunashindwa kutokana na upungufu wa fedha, naamini mipango ikikaa sawa tutawapeleka kila mkoa," alisema Nyoni.

Kiongozi huyo alikiri sasa kuna ongezeko kubwa la watu wanaotaka kuufahamu mchezo huo tofauti na ilivyokuwa katika siku zilizopita.

"Sasa hivi muamko wa mchezo huo unazidi kukua kwa kasi, ukilinganisha na miaka mingine, watu walikuwa wanauogopa mchezo huu kupita kiasi," Nyoni alisema.

# Wachezaji KMC kwenda 'likizo'

Na Shufaa Lyimo

UONGOZI wa KMC FC umesema utawapa wachezaji wake mapumziko mafupi baada ya kufanya mazoezi magumu mfulululizo, imeelezwa.

Kocha Mkuu wa KMC FC, Haruna Hererimana, alisema amewapa wachezaji wake mapumziko ya siku tatu na hii inatokana na uchovu waliopata baada ya kufanya mazoezi magumu mfululizo.

Hererimana alisema mapumziko hayo yatawasaidia kupumzisha miili na kurejea wakiwa na nguvu mpya.

"Lengo langu ni kushika nafasi za juu katika msimamo wa ligi, vile vile hatutaki kushuka daraja," alisema Hererimana.

Aliongeza kwa sasa wanajiandaa kukutana na Ruvu Shooting katika mchezo utakaochezwa June 20, mwaka huu na wanafahamu mechi hiyo haitakuwa rahisi.

"Tunaahidi kurudi kivingine, ninaipa umuhimu mkubwa Ruvu Shooting, nafahamu ina wachezaji wazuri, binafsi nahitaji kuendelea kubakia katika Ligi Kuu," Hererimana alimaliza.

# Michezo

Jumamosi Juni 13, 2020

**Nipashe**



## Zidane atangaza kumhitaji Kante

HABARI UK 22



Mshambuliaji wa Yanga, Ditram Nchimbi (kushoto), akiwa na winga, Mrisho Ngasa, katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Fresho mkoani Shinyanga jana asubuhi. **PICHA: YANGA**

## Simba yapanga kuimaliza Ruvu

**Na Somoe Ng'itu**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, wamesema mawazo, akili na nguvu zao zote wamezielekeza katika mchezo dhidi ya Ruvu Shooting utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, aliliambia gazeti hili kikosi chao kiko kamili na tayari kuendelea na safari ya kuwania ubingwa wa ligi hiyo ya juu nchini.

Rweyemamu alisema wanafahamu mechi zote zilizosalia ni ngumu, lakini wao malengo ya kutetea taji hilo waliyonayo, hayajabadilika na wataendelea kupambana hadi mwisho.

"Hakuna mechi rahisi katika ligi, lakini Simba ilipofikia si mahali unapoweza kutufananisha na wengine, sisi tunaangalia tulichokidhamiria, tutajipanga kuhakikisha tunatimiza malengo yetu, ingawa haitakuwa kazi nyepesi," Rweyemamu alisema.

Aliongeza kila mchezaji amedhamiria kupata namba katika kikosi, hivyo ushindani na ubora wanaouonyesha kwenye mazoezini, unalifanya benchi la ufundi kuwa na kazi nyepesi.

Simba itashuka uwanjani kesho kucheza dhidi ya 'Maafande' wa Ruvu Shooting, ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa kishindo wa mabao 8-0, ambao waliupata walipocheza na Singida United.

# YANGA, MWADUI HATUMWI MTOTO

### ●●●Mkwasa atamba mipango na mikakati ya kuwafunga 'wachimba dhahabu' imekamilika, Morisson awazimia simu viongozi...

**Na Isaac Kijoti**

HATIMAYE mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zinatarajia kurejea nchini kuanzia leo baada ya ligi hiyo kusimama kwa zaidi ya miezi miwili kwa lengo la kujikinga na maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), vilivyotikisa kila kona duniani.

Mshikemshike huo leo utashuhudia mechi mbili ambapo kwenye Uwanja wa CCM, Kambarage mkoani Shiyanga wenyeji Mwadui FC watawakaribisha Yanga wakati Namungo FC itakuwa ugenini kuwakabili Coastal Union kwenye Uwanja wa CCM, Mkwakwani jijini, Tanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Boniface 'Master' Mkwasa, alisema kikosi chake kiko imara na wamekwenda Shinyanga kwa kazi moja ya kuchukua pointi tatu muhimu.

Mkwasa alisema katika mchezo wa leo, Yanga itawakosa nyota wake wanne akiwamo nahodha, Papy Tshishimbi ambaye ni majeruhi, Eric Kabamba, Ally Ally na mshambuliaji, Bernard Morisson ambaye hakupatikana katika timu yake jana asubuhi.

"Tunamshukuru Mungu tumefika salama Shinyanga, tumekuja huku kwa ajili ya kutafuta ushindi, kuna wachezaji baadhi tutawakosa, mmojawapo ni Tshishimbi ambaye ni majeruhi, lakini vile vile ana kadi tatu za njano, hata angekuja, asingeweza kucheza, " alisema Mkwasa.

Aliongeza kikosi chake kimejipanga kukabiliana na ushindani katika mchezo huo na wanafahamu haitakuwa mechi rahisi.

Naye Ofisa Uhamasishaji wa timu hiyo, Antonio Nugaz, alisema Kocha Mkuu, Luc Eymael na mshambuliaji, David Molinga, waliwasili Shinyanga jana na kuungana na kikosi cha Yanga kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa leo.

Nugaz alisema uamuzi wa kumsafirisha Molinga ulifanywa na Eymael na hiyo imetokana na 'kuyeyuka' kwa Morisson ikiwa ni saa chache kabla ya kuanza safari ya kuelekea Shinyanga.

"Yale yaliyokuwa yanatokea, sintofahamu, tuyaache, ninataka tufanye kazi, twende mbele, tufikiri ushindi," Nugaz alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Mwadui FC, Khalid Adam, alisema kikosi chake kimejipanga vizuri kukutana na Yanga na wataingia uwanjani kwa tahadhari kwa sababu wanafahamu wapinzani wao ni timu kubwa.

"Tunaingia kwa tahadhari kwa sababu wapinzani wetu wametuzidi kila kitu, lazima tujipange kikamilifu," alisema Khalid.

Aliongeza kila wanapokutana na timu kongwe, wachezaji wake wanakuwa na morali ya juu na wanaahidi kuongeza umakini ili malengo ya kutopoteza mchezo yatimie.

"Tumejipanga na tuko tayari kukutana na Yanga hapo kesho (leo), tunajua mchezo utakuwa mgumu, kila upande unahitaji pointi tatu ili kujiimarisha kwenye msimamo," alisema kocha huyo.

Aliwataka mashabiki wa timu hiyo na wadau wa soka wa Shinyanga kujitokeza kuishangilia Mwadui kwa sababu wamedhamiria kusaka ushindi ili wapate pointi zitakazowabakisha kwenye Ligi Kuu Bara.

"Naomba mashabiki wetu waje uwanjani wakiwa wamejikinga na vifaa vya kuzuia ugonjwa wa corona, tunatakiwa kufuata maagizo ya serikali na tuhakikishe tunajiepusha na msongamano usiotakiwa na," Khalid alisema.

Yanga yenye pointi 51 imecheza mechi 27, itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kuchapwa bao 1-0 na KMC FC katika mchezo wake wa mwisho wakati Mwadui ilifungwa goli 1-0 na JKT Tanzania.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >